# FANI KATIKA KAZI TEULE ZA MOHAMMED SAID ABDULLA

**NA**


**AMISI YUNNY**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**DESEMBA, 2023**

## UNGAMO

Kazi hii ni yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.



Sahihi________________________ Tarehe: 10-07-2023

**AMISI YUNNY**

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.



Sahihi________________________ Tarehe: 10-07-2023

**PROF. EVANS M. MBUTHIA**

(Msimamizi)



Sahihi________________________ Tarehe: 10-07-2023

**DR. SANJA, L. W. LEONARD**

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku wazazi wangu wapendwa Apollo Otemba Asionyi na Peninah Noel Asionyi pamoja na mwanangu Joe Arthur. Himizo kutoka kwa baba mzazi na mafunzo kutoka kwa mama ndiyo yaliyonifikisha katika ngazi hii ya kiakademia. Mungu awabariki sana.

## SHUKRANI

Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hekima kuendeleza masomo yangu katika utu uzima wangu. Shukrani za dhati pia ni kwa wasimamizi wangu, Prof. Evans M. Mbuthia na Dkt. Leonard Sanja walionielekeza vyema na kunisaidia kujipanga ili nikamilishe kazi hii kwa wakati uliotakikana. Nawashukuru wahadhiri wote walionifundisha tangu nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi mnano mwaka wa 2017. Wahadhiri hawa ni Prof. Evans Mbuthia, Prof. Iribe mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Rayya Timammy, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Leonard Sanja na Dkt. Basilio Mungania. Natoa shukrani za kipekee kwa Prof. Rayya Timammy kwa kuchukua hatua ya kutukutanisha na mwanafasihi Prof. Kithaka Wa Mberia kwani maelezo yake kuhusu fasihi yalinifaa sana wakati wa kuandika kazi hii.

Ningependa kushukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili. Baadhi yao ni Simon, Kirui, Agatha, Deon, Kangethe, Meshack, Oliver, Petronila na wengineo. Ningependa pia kuwashukuru wazazi wangu wapendwa, baba yangu Apollo Otemba Asionyi na mama yangu Peninah Noel Asionyi kwa kunipa malezi na mafunzo mema nilipokuwa mdogo hadi nilipohitimu shahada yangu ya kwanza. Pia walinipa mawaidha mema na motisha katika masomo yangu. Aidha namshukuru mwanangu mpendwa Joe Arthur ambaye alinivumilia kwa muda ambao sikuweza kushirikiana naye aliponihitaji haswa alipokuwa likizoni nami chuoni nikisoma.

Ningependa aidha kuwashukuru rafiki yangu, David ambaye alichangia pakubwa katika kunisaidia kulipa karo ya chuo na kunipa motisha na mawaidha mema. Mungu akubariki sana. Shukrani kwa ndugu zangu Florida, Grace, Pamela, Hannington, Alice, Mercy na wapwa wangu Sydney, Owen, Lyne, Melody, Nicole, Elsey, Alvin, Quintonne, Fortune, Bishop, Bright, Kendyll, Kaelynn, Kaycee kwa kunipa motisha na kuniombea.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza msuko, usimulizi na matumizi ya lugha katika kazi teule za M. S. Abdulla: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007). Malengo ya utafiti huu yalikuwa yafuatayo: kudhihirisha aina za misuko katika riwaya teule, kubainisha namna usimulizi ulivyoshughulikiwa katika riwaya teule na kuonyesha matumizi maalum ya kunga za lugha katika riwaya zilizoteuliwa. Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo: ni misuko ya aina gani ambayo M. S. Abdulla anaitumia katika riwaya zake teule? Usimulizi umeshughulikiwa vipi katika riwaya teule za M. S Abdulla? Na je, M. S. Abdulla anatumia kunga zipi za lugha katika riwaya zake teule? Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, tulitumia Nadharia ya Naratolojia na ya Umitindo. Huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani. Tulisoma vitabu, makala, majarida na tahakiki mbalimbali pamoja na habari za mitandaoni kuhusu kazi za M. S. Abdulla.Kupitia mbinu ya usomaji na unakili, tuliandika na kunukuu data zote muhimu na kuziainisha kulingana na malengo ya utafiti huu kabla ya kuichanganua na kudhihirisha matokeo ya utafiti kwa njia ya kimaelezo. Utafiti ulidhihirisha ya kuwa, riwaya teule za M. S. Abdulla zinatumia misuko, usimulizi na kunga za lugha kwa njia changamano ili kukuza maudhui na dhamira kwa njia inayombainishia msomaji mtazamo wa mwandishi kuhusu matukio mbalimbali katika jamii ya kazi hizi katika nyakati tofauti zilizolengwa. Utafiti huu umewezesha kueleweka kwa kina kwa riwaya teule za mwandishi huyu na masuala anayoyashughulikia kwa msomaji wa kawaida wa fasihi na pia kuibua mitazamo mpya wa kazi hii kwa mhakiki.

## YALIYOMO


ANWANI YA MADA ........................................ i

UNGAMO ........................................ ii

TABARUKU ........................................ iii

SHUKRANI ........................................ iv

IKISIRI ........................................ v

YALIYOMO ........................................ vi

**SURA YA KWANZA:MSINGI WA UTAFITI ........................................ 1**

1.0 Usuli wa Mada ........................................ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........................................ 2

1.2 Maswali ya Utafiti ........................................ 3

1.3 Malengo ya Utafiti ........................................ 3

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................ 3

1.5 Upeo na Mipaka ........................................ 4

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................ 4

1.7. Msingi wa Kinadharia ........................................ 5

1.7.1 Nadharia ya Umitindo: Utangulizi ........................................ 5

1.7.2 Nadharia ya Umitindo ........................................ 6

1.7.3 Mihimili ya Nadharia ya Umitindo ........................................ 8

1.8 Nadharia ya Naratolojia ........................................ 8

1.8.1 Utangulizi ........................................ 9

1.8.2 Nadharia ya Naratolojia ........................................ 9

1.9 Mbinu za Utafiti ........................................ 12

1.9.1 Ukusanyaji wa Data ........................................ 12

1.9.2 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo ........................................ 13

**SURA YA PILI:MSUKO KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007) ........................................ 14**

2.0 Utangulizi ........................................ 14

2.1 Aina za Misuko ........................................ 14

2.1.1 Matumizi ya ki-Anakroni ........................................ 15

2.1.2 Msuko Kioo katika Riwaya Teule ........................................ 22

2.2.2 Msuko Mwanzo-Kipeo katika Riwaya Teule ........................................ 29

2.2 Hitimisho ........................................ *29*

**SURA YA TATU:USIMULIZI KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007) ....................................................................31**

3.0 Utangulizi....................................................................................31

3.1 Usimulizi kwa Ujumla ....................................................................31

3.2 Daigesia.........................................................................................33

3.3 Usimulizi wa Mimesia ....................................................................38

3.4 Usimulizi Maizi ..............................................................................42

3.5 Hitimisho.......................................................................................44

**SURA YA NNE:KUNGA ZA LUGHA KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007)...............................................................45**

4.0 Utangulizi....................................................................................45

4.1 Matumizi ya Lugha katika Kazi za Kifasihi .......................................45

4.2 Matumizi ya Methali.......................................................................45

4.2.1 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Thamani ya Kutenda Wema.........46

4.2.2 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Imani za Kishirikina.....................46

4.2.3 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Haja ya Kufanya Upelelezi Bora..47

4.2.4 Matumizi ya Methali Kutoa Nasaha kwa Wanajamii................................47

4.3. Misemo na Nahau ..........................................................................48

4.3.1 Matumizi ya Misemo Kueleza Ufanisi Katika Kilimo...............................48

4.3.2 Matumizi ya Misemo katika Kuzungumzia Masuala ya Urithi..................49

4.3.3 Matumizi ya Misemo katika Kueleza Hali Anuwai za Kijamii..................49

4.3.4 Matumizi ya Misemo katika Kueleza Hali ya Kuwekana Kimada .............50

4.4. Matumizi ya Tashihisi.....................................................................50

4.4.1 Matumizi ya Tashihisi Kuonya Kuhusu Hulka na Ufuska ..........................50

4.4.2 Matumizi ya Tashihisi Kueleza Hali ya Seyyid Ahmed.............................51

4.4.3 Matumizi ya Tashihisi Kusisitiza Wingi wa Vyakula ................................51

4.4.4 Matumizi ya Tashihisi Kutoa Maelezo kwa Kitafsili.................................51

4.5. Matumizi ya Sitiari .........................................................................52

4.5.1 Matumizi ya Sitiari katika Kufafanua Imani za Kidini na Itikadi za Kishirikina ..........................................................................................52

4.5.2 Matumizi ya Sitiari katika Kusisitiza Masuala Yanayoambatana na Urithi 53

4.6. Matumizi ya Takriri .........................................................................53

4.6.1 Matumizi ya Takriri Kusisitiza Udhati wa Uchunguzi...............................54

4.6.2 Matumizi ya Takriri Kuibua Taswira Kamili ya Mandhari ya Kisimani ....54

4.7. Matumizi ya Tabaini ....................................................................................55
4.7.1 Matumizi ya Tabaini Kuelezea Umbo la Spekta Seif.................................55
4.8. Matumizi ya Tashbihi ......................................................................................55
4.8.1 Matumizi ya Tashbihi Kueleza Maumbile ya Mwana wa Giningi.............56
4.8.2 Matumizi ya Tashbihi Kueleza Maumbile ya Ali Makame ........................56
4.8.3 Matumizi ya Tashbihi Kuonyesha Umuhimu wa Uwajibikaji Kazini ........56
4.8.4 Matumizi ya Tashbihi katika Kutoa Nasaha...............................................57
4.8.5 Matumizi ya Tashbihi Kubuni Taswira ya Mizozo ya Kinyumbani ...........57
4.9 Matumizi ya Tanakali za Sauti ..........................................................................57
4.9.1 Matumizi ya Tanakali za Sauti kueleza Hulka za Kiupelelezi za Bwana Msa ....................................................................................................58
4.9.2 Matumizi ya Tanakali za Sauti Kuelezea Kilichojiri Pindi Mwana wa Giningi alipouwawa....................................................................................58
4.10 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi ....................................................................59
4.10.1 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi Kueleza Kutoroka kwa Jamila ............59
4.10.2 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi Kueleza Wasiwasi wa Seyyid Ahmed .59
4.10.3 Matumizi ya Uzungumuzi Nafsia Kumweleza Mwana wa Giningi Kuhusu Urithi...........................................................................................................60
4.11 Matumizi ya Taswira .......................................................................................61
4.11.1 Matumizi ya Taswira Kuonyesha Uwajibikaji wa Maafisa wa Polisi.......61
4.11.2 Matumizi ya Mandhari Kuibua Tofauti za Kitabaka ...............................62
4.12 Hitimisho.........................................................................................................63
**SURA YA TANO:MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.........................................................................................64**
5.1 Utangulizi...........................................................................................................64
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ......................................................................64
5.3 Matokeo ya Utafiti .............................................................................................66
5. 4 Mchango wa Utafiti ..........................................................................................67
5.5 Mapendekezo .....................................................................................................67
**MAREJELEO .......................................................................................................68**

# SURA YA KWANZA
# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 Usuli wa Mada

Uwezo wa mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake kwa njia ya kusisimua hutegemea namna ambavyo maudhui na dhamira yanavyowasilishwa kupitia kazi ya kifasihi inayoshughulikiwa (Simpson 2004:2). Fani tofauti ikiwemo mbinu za lugha hudhihirisha upekee wa mtunzi na jinsi gani anavyotofautiana na watunzi wengine (Leech 1969). Leech anadhihirisha ya kuwa, kila mwandishi wa kazi za fasihi ana mtindo wake ambao ni tofauti na wa waandishi wengine. Pia, anadhihirisha ya kuwa, mtindo ni mtu mwenyewe na jinsi anavyojibidiisha kuitumia lugha kupitisha ujumbe kwa hadhira anayoinuia. Hii ina maana ya kwamba, mbinu anazozitumia mwandishi wa fasihi huweza kuwa kiungo muhimu cha kuzungumzia maudhui kwa njia ya kuvutia na hata kumsisimua msomaji wa kazi husika.  Ni kutokana na ufahamu huu ambapo kila kazi ya kisanaa inastahili kuchunguzwa kipekee ili kubainisha ubora wa kazi husika. Kila mtunzi wa fasihi ana namna yake ya kuteua aina ya msuko na aina ya usimulizi kulingana na masuala ambayo anakusudia kuyazungumzia katika kazi yake. Muktadha wa kazi pamoja na malengo ya mwandishi huchangia pakubwa sababu za kuteua aina fulani ya msuko na usimulizi. Mwandishi hufanya hivyo pia kuhusiana na matumizi ya lugha.  Hili huathiri namna kila kazi inavyofasirika na msomaji wa kazi ya kifasihi. Vitushi na usawiri wa wahusika ni viungo muhimu vinavyotumiwa na mtunzi kuendeleza dhamira na maudhui. Vipengele hivyo kwa wingi huathiriwa kutokana na aina ya msuko, usimulizi na matumizi ya lugha zinazotumiwa na mwandishi. Hii ndio sababu wasanii wawili wanaweza kutumia fani na mbinu za lugha zinazofanana lakini malengo yakawa tofauti ama athari zake kwa msomaji zikawa tofauti baina ya kazi moja na nyingine.

Fani na mtindo wa lugha ni nyenzo muhimu ambazo zinafumbata dhamira kuu ya mtunzi (Mohamed 1995). Dhamira na maudhui katika kazi yoyote ya kifasihi hudhibitiwa na fani pamoja na matumizi ya lugha ambayo ni mwafaka. Mwandishi huteua fani kulingana na hadhira anayoilenga. Mohamed vilevile anakubaliana na fasiri ya mtindo kama mtu binafsi. Matumizi ya lugha ya kitamathali kama methali ama matumizi ya majazi yanabainika sana katika kazi za S. M. Abdulla kupitia wahusika kama, Fundi Magungu na wengine (*Kisima cha Giningi*). Fani na matumizi ya lugha mahsusi huathiri namna msomaji wa fasihi anafasiri maana ya kazi husika.

Katika kazi husika, Fundi Mangungu anadhihirisha kuwepo kwa ushirikina katika jamii ya Giningi.

Fasihi huwa ndilo jukwaa la kudhihirishia matumizi ya lugha na vipengele vingine vya fani katika mazingira mbalimbali (Simpson 2004:2). Ni muhimu basi kuzichunguza kazi za kifasihi kibinafsi kwa maana ujumbe unavyowasilishwa hutegemea mbinu mahsusi za kila mwandishi. Mtindo wa lugha husaidia katika kusisitiza ujumbe na kubainisha tukio moja na lingine. Pia, humsaidia msomaji wa fasihi kutambua ni masuala yapi mwandishi anayoyatilia maanani na kwa nini. Fani na matumizi ya lugha basi huweza kumsaidia mhakiki wa kazi ya kifasihi kubainisha matukio makuu ya kazi na wajibu wa wahusika katika kazi inayochunguzwa. Ili kufinyanga kazi ya kifasihi kiusanii na kuipa ushawishi unaofaa kwa hadhira lengwa, mwandishi wa fasihi hana budi kuwa mwangalifu katika masuala ya usimulizi na msuko wa vitushi (Wamitila 2003:39). Anachosema Wamitila ni kwamba, kila mwandishi hubainika kifasihi na ndiposa kuna haja ya kuichunguza kila kazi ya mwandishi fulani kipekee bila kuwajumulisha kiholela.

Fani na msuko huendana pamoja kwa kuwa hujengana (Senkoro 1982). Hii ni kwa sababu, matumizi ya lugha katika kazi ya kifasihi huteuliwa kutegemea msuko wa vitushi na namna mwandishi husika anavyotaka kuwasilisha ujumbe kwa msomaji wake (Wafula, 2007). Mbinu za lugha na usimulizi huongeza kasi, kubainisha wahusika na kudhihirisha namna wahusika hao wanavyobadilika kulingana na wakati kimatukio (Wamitila, 2003). Fani na matumizi ya lugha huathiri namna msomaji wa fasihi anavyozielewa kazi husika (Wales, 2011:20). Kuchunguza msuko, usimulizi na matumizi ya lugha basi ni njia mwafaka ya kuielewa kazi ya mwandishi fulani wa kazi za kifasihi kwa kina. Utafiti huu unamulika riwaya za, *Kisima cha Giningi (1968)* na *Kosa la Bwana Msa* (2007) za M. S. Abdulla kwa mtazamo tulioueleza.

### 1.1 Tatizo la Utafiti

Matumizi ya lugha ya kitamathali huathiri namna msomaji wa fasihi anavyolewa kazi husika. Mbinu ambazo mtunzi huteua ili kumwathiri msomaji kihisia huwa ni muhimu katika kufanikisha usanii ulio bora (Senkoro 1988). Uwezo wa mtunzi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa kwa njia ya kusisimua hutegemea msuko wa vitushi, usimulizi na kunga za lugha. Utafiti huu ulichunguza msuko, usimulizi na matumizi ya lugha katika kazi teule za M. S. Abdulla: *Kisima cha Giningi (1968)* na

*Kosa la Bwana Msa* (2007) kwa lengo la kuweka bayana dhamira na maudhui ya kazi husika kwa msomaji wa kawaida wa kazi teule za mwandishi huyu. Kwa kufanya hivyo, uchunguzi huu unalenga kudhihirisha umahususi na upekee wa kujieleza wa mwandishi M. S. Abdulla katika vipengele tulivyovishughulikia kimtindo na kifani. Kuchunguza matumizi ya lugha, msuko na usimulizi katika kazi za fasihi huwa ni njia ya kuifumua kazi husika kwa hadhira pana ili kufurahia kazi yenyewe kutokana na kiwango chake cha ujumi pamoja na kuwaathiri kihisia kama anavyokusudia mtunzi (Wales (2011:20).

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni misuko ya aina gani ambayo M. S. Abdulla anaitumia katika riwaya zake teule?

ii) M. S. Abdulla anatumia usimulizi wa aina gani katika riwaya zake teule?

iii) Kunga za lugha zinatumika kwa njia gani na M.S. Abdulla katika riwaya zilizoteuliwa?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

i) Kudhihirisha aina za misuko katika riwaya teule za M. S. Abdulla.

ii) Kudhihirisha aina ya usimulizi anaoutumia M. S Abdulla katika riwaya zake teule.

iii) Kuonyesha namna kunga za lugha zilivyotumika kwa njia maalum katika riwaya zilizoteuliwa na M.S. Abdulla.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Msuko huhusu mtiririko wa vitushi katika kazi za kifasihi na namna vinavyofuatana. Msuko pia unahusisha matukio na visababishi vyake. Mbinu na fani ambazo mwandishi wa fasihi anazitumia katika kazi yake huathiri namna ujumbe unavyoupokelewa. Msomaji huathiriwa kutokana na namna ujumbe ulivyowasilishwa kwake pamoja na kwamba fani husaidia katika kudhibiti ujumbe na kuinua kiwango cha ujumi katika kazi husika. Msuko huwa muhimu katika kazi yoyote ya kifasihi. Hufungamanisha maudhui na dhamira ya mwandishi pamoja na kudhihirisha mbinu za lugha ambazo mtunzi huzitumia pamoja na namna anavyowasiliana na hadhira

yake (Senkoro 1988). Kwa hivyo tulimulika vipengele hivyo katika kazi teule za M. S. Abdulla ili kudhihirisha upekee wake kama mwandishi wa riwaya.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu ulijikita katika kazi teule za M. S. Abdulla ambazo ni: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007). Aidha tulijikita katika vipengele vya: msuko na usimulizi na mbinu za lugha pekee katika riwaya hizo. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti wetu kwa kuongozwa na nadharia za Umitindo na Naratolojia

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Lugha ina dhima kubwa katika uwasilishaji wa maana katika kazi za kifasihi (Kitsao 1975). Kitsao alishughulikia mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili na kuonyesha kwamba, kategoria mbalimbali za maneno zinaweza kuathiri maana mbalimbali zinavyopatikana na kumdhihirikia msomaji wa kifasihi. Kazi yake ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu inahusiana na mihimili ya nadharia ya Umitindo ambayo iliongoza utafiti wetu. Kazi yake ilitupa mwongozo wa kinadharia na kutusaidia kulielewa suala letu la utafiti kwa kina. Tofauti ya kazi yake na yetu ni kuwa, yeye alishughulikia kategoria za maneno pekee lakini kazi yetu ilishughulikia msuko, usimulizi na kunga za lugha kwa ujumla na kubainisha athari zake katika kazi za M.S. Abdalla.

Senkoro (1982), alishughulikia uhakiki na nadharia ya ushairi kwa ujumla pamoja na mtindo wa lugha katika utunzi wa mashairi na namna ujumbe unavyoifikia hadhira kwa njia ya kusisimua. Kwa mujibu wake, msuko ni sehemu muhimu ya fani kwani msuko wa kazi za kifasihi huwa na athari kubwa kwa kazi husika. Mbinu za lugha na fani kwa ujumla huathiri usimulizi wa kazi za kifasihi katika masuala kama dhamira, maudhui na msuko wa vitushi. Kwa njia hiyo, kazi husika huwa na athari kubwa kwa msomaji. Usimulizi na msuko ni mojawapo wa vipengele ambavyo sisi tulivishughulikia katika utafiti wetu. Mawazo ya Senkoro yalimpa mtafiti undani wa kinadharia wa suala lake wakati wa kusoma maktabani na uainishaji wa data kabla ya kuichanganua.

Ndung'u (1996) alishughulikia fani katika riwaya za Katama Mkangi za, *Ukiwa, Mafuta* na *Walenisi*. Yeye alijikita zaidi katika usawiri wa wahusika na namna wanavyochangia katika uendelezaji wa dhamira na maudhui. Kazi yetu ilihusu zaidi

msuko, usimulizi na lugha ilivyotumika na kuonyesha athari yake kifani katika uelewekaji wa kazi za mwandishi M S. M, Abdalla.

Kairu (2005) alishughulikia masuala ya watoto na mtindo katika maandishi ya Ken Walibora. Mbali na mtindo, alishughulikia maudhui na usimulizi kwa kiwango fulani. Kazi yake ilimpa mtafiti undani wa suala lake Kinadharia. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na yetu kinadharia. Kairu alitumia nadharia ya Uhalisia ilhali kazi yetu ilitumia nadharia ya Umtindo na Naratolojia.

Ongarora (2007) alishughulikia mtindo katika Arusi ya *Buldoza na Hadithi Nyingine.* Ingawa kazi yake ilishughulikia suala la mtindo, inatofautiana na yetu kwa kuwa yeye alijikita katika utanzu wa hadithi fupi ilhali kazi yetu ilihusu utanzu wa riwaya.

Uchunguzi wa Sanja (2012) ulilenga riwaya mbili *Paradiso* na *Kala Tufaha* kwa kutumia nadharia ya Uhistoria Mpya wa Kiswahili. Alishughulikia maudhui na kufafanua baadhi ya mbinu za lugha katika kazi yake. Kazi yake ilitupa undani wa kinadharia wa suala letu kwani kunga za lugha ni kati ya maswala tuliyoyashughulikia. Muthoni (2014) alichunguza maudhui na mtindo katika *Tikitimaji* ya Wamitila. Kazi yake iiliwiana na yetu kuhusu usimulizi. Hata hivyo, ilitofautiana na yetu kwa kuwa tulichunguza matini tofauti.

Mbuthia na Iribe Mwangi (2014) walizungumzia mbinu za lugha katika hadithi fupi katika diwani kadhaa za Kiswahili. Lengo lao lilikuwa kudhihirisha jinsi ambavyo, waandishi wa hadithi fupi walivyopevuka kisanaa na hasa katika matumizi ya mbinu za lugha kama methali, maswali ya balagha na jazanda. Mawazo yao kuhusu mtindo wa lugha katika hadithi fupi za Kiswahili yalimpa mtafiti undani wa kinadharia kuhusiana na suala lake la utafiti.

### 1.7. Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia za Umitindo na Naratolojia. Nadharia hizi zinajengana ili kumulika maswala ya kimtindo na usimulizi yanayoshughulikiwa katika kazi hii.

#### 1.7.1 Nadharia ya Umitindo: Utangulizi

Utafiti wetu ulitumia nadharia ya Umitindo iliyochangiwa pakubwa na Leech (1969) kwani suala letu linahusiana na vipengele vya msuko, usimulizi na matumizi ya lugha. Vipengele husika vinahusiana na mtindo katika kazi za kifasihi moja kwa

moja. Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ina mihimili ambayo ilitusaidia kuchunguza suala letu la utafiti kikamilifu na kutuwezesha kutimiza malengo ya utafiti huu. Malengo ya kazi humsukuma msanii kuamua kuteua aina ya nadharia zitakazoongoza kazi yake katika juhudi za kuwasilisha ujumbe kwa njia bora iwezekanavyo.

### 1.7.2 Nadharia ya Umitindo

Dhana ya Umitindo hutumiwa kurejelea uchunguzi wa lugha na namna mbalimbali ya kuelezea matukio katika matini za kifasihi (Wamitila 2003:39). Lugha ya kitamathali aghalabu hutokana na matumizi ya lugha ya kawaida. Ukawaida huo huibua ukiushi na ukiushi huo huibua upekee wa matumizi ya lugha. Ukiushi wa lugha hutokea katika viwango mbalimbali vinavyohusu kategoria zifuatazo: leksia, sarufi na semantiki (Leech 1969). Kunga za lugha kama vile jazanda, misemo, nahau na taswira pamoja na tashbihi huanza kama lugha ya kawaida tu. Muktadha na matumizi huweza kutofautisha na pia kupanua maana zinazolengwa na mwandishi wa kazi ya kifasihi. Ni dhahiri basi kuwa lugha ya kifasihi chanzo chake ni lugha ya kawaida. Kazi ya fasihi hutumia mbinu mbalimbali kama jazanda, tashhisi, tashbihi, taharuki, maswali ya balagha na mbinu nyingine nyingi za lugha. Mbinu hizo hutokana na msuko wa vitushi na aina ya usimulizi katika kazi husika.

Nadharia ya mtindo inahusu namna mwanafasihi anavyosanii lugha katika kazi yake (Leech 1969:02). Kauli yake inadokeza kuwa, kuna upekee katika matumizi ya lugha unaodhihirishwa na watunzi mbali mbali. Kwa hivyo, kulingana na nadharia hii, kazi tofauti za waandishi tofauti zinaweza kutofautishwa katika misingi ya mitindo iliyotumika katika kazi husika. Mtindo wa mwandishi huamuliwa na malengo yake na maswala anayotaka kuibua katika kazi yake.

Matumizi ya lugha ya kawaida kwa njia maalum huweza kuibua mitindo tofauti ambayo huwatofautisha waandishi. Leech anabainisha umuhimu wa muktadha katika kuteua matumizi ya lugha ambayo yanaafiki kazi fulani ya kifasihi kuhusiana na msuko wa vitushi na namna ya usimulizi katika kazi husika. Leech (1969) anaeleza:

> Umitindo ni uhakiki na ufasiri wa kazi za kifasihi katika mtazamo wa kiisimu. Kama taaluma, inafungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan stiari, taswira, kinyume, kinaya, usambamba na

> jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. (u.k:2-6)

(Tafsiri ni yetu)

Kulingana na dondoo hili, kuna uhusiano baina ya lugha ya mwandishi na aina ya kazi. Lugha ya kawaida hugeuka na kupewa upekee na aghalabu kuwa ya kitamathali. Mtindo hujibainisha pia katika dayalojia. Lugha ya kuzungumzwa hutegemea lengo, msemaji na mlengwa. Mtindo mmoja wa lugha unaweza kuibua maana ya kina ya kazi ya kifasihi. Hiyo ndiyo lugha ambayo Leech anaiita lugha ya kitamathali. Yeye anaeleza masuala kama lafudhi, matumizi ya msamiati wa kilahaja na lugha katika mazingira mbalimbali kama ishara za umtindo katika matumizi ya lugha katika viwango mbalimbali. Lafudhi ina umuhimu mkubwa inapotumika katika kazi ya kifasihi. Lafudhi huweza kumtambulisha mhusika mmoja na mwingine kwa njia kama alikozaliwa, mazingira na hata kwa masuala kama umri ama lugha yake ya kwanza. Pia, inaweza kuonyesha hadhi yake katika jamii.

Kulingana na nadharia ya Umitindo, kila rejista ina upekee wake. Hali hiyo ndiyo ibainishayo sajili ama mkutadha binafsi. Mathalani Lugha ya matangazo ya kibiashara haiwezi kulingana na lugha inayotumika katika mazingira ya mahakama. Kila kazi ya kifasihi huongozwa na muundo au sifa za kiutanzu. Mbinu kama vile usimulizi na msuko huathiri matumizi ya lugha. Kila mtindo wa mwandishi binafsi hujidhihirisha kwa njia ya kipekee na katika mkutadha maalum. Umitindo hubainisha taratibu zinazotumika katika mawasiliano mbalimbali kutegemea ujumbe na namna unavyowasilishwa kwa msomaji. Kadri ambavyo mtunzi wa fasihi hujibidiisha kutumia mitindo mbalimbali kupitisha ujumbe wake ndivyo anavyoweza kujitokeza na mitindo mbalimbali katika kazi yake.

Kulingana na nadharia ya Umitindo, umbo la kazi vilevile linaweza kuathiri matumizi ya lugha na uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira. Kwa mfano, ufasiri wa shairi hutegemezwa arudhi na maudhui yanayojadiliwa. Hali hii huifanya lugha ya ushairi kuwa lugha ya kipekee kimtindo. Matini inavyoaandikwa hutegemezwa miktadha maalumu ambayo pia huibua upekee wa matumizi ya lugha (Crystal na Davy 1969:10) Kwa hivyo, uelewa wa matini fulani humlazimisha msomaji au mhakiki kuzingatia muktadha wa matumizi ili kuweza kubainisha maana iliyokusudiwa na mwandishi. Kulingana na Harries (2009), lengo la kutumia mtindo fulani ni

kufanikishwa uwasilishaji wa ujumbe kwa kutumia fani za aina mbalimbali. Pia, huwa na lengo la ujumi ambao pia ni kitambulisho cha matini za kifasihi.

### 1.7.3 Mihimili ya Nadharia ya Umitindo

Baada ya kuisoma nadharia ya Umitindo, tuliteua mihimili ifuatayo kuongoza utafiti wetu:

1. Mbinu za lugha na fani kwa ujumla huathiri namna ujumbe humfikia msomaji wa kazi ya kifasihi. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuchunguza matumizi ya lugha na fani katika riwaya teule za M.S. Abdulla ilimsaidia mtafiti kuchanganua data kuhusu mbinu kama vile sitiari, jazanda na maswali ya balagha.
2. Matumizi ya lugha na fani huhusiana na jinsi mwandishi wa fasihi anavyoibua na kuzungumzia maudhui na dhamira mbalimbali katika kazi yake. Mhimili huu ulitusaidia katika kuchanganua data kuhusu matumizi ya fani na lugha pamoja na kueleza athari zake katika vitabu teule.

3. Mtindo humbainisha mtunzi wa kazi za kifasihi pamoja na waandishi wengine wa kazi ya bunilizi. Mhimili huu ulisaidia katika kuchunguza vipengele vya fani na lugha vilivyombainisha mwandishi teule na kazi nyingine zake na waandishi wengine.

Kutathmini fani na matumizi ya lugha katika kazi teule za mwandishi wa kifasihi ni njia mojawapo ya kudhihirisha upekee wa mtunzi. Jinsi kila mwandishi anavyotumia msuko, usimulizi, anavyowasawiri wahusika pamoja na mitindo mbalimbali ya lugha anayotumia humtofautisha na wasanii wengine na pia hutofautisha kazi tofauti za kisanii.

## 1.8 Nadharia ya Naratolojia

Nadharia ya naratolojia ina mahusiko badilia ambayo hufafanua aina tofauti za usimulizi na mbinu ainati za usimulizi. Katika sehemu hii tutajikita kati baadhi ya mbinu ambazo zinadhihirika katika riwaya zilizoteuliwa.

### 1.8.1 Utangulizi

Kama anavyoshadidia Wamitila (2002:139), nadharia hii iliwekewa msingi na Plato katika kazi yake ya, *Republic*. Plato alizungumzia usimulizi katika hali ya *mimesia* na *Daigesia*. Katika *mimesia*, msimulizi hajitokezi waziwazi. Katika daigesia, msimulizi anabainika kwani anajitokeza waziwazi. Wengine waliochangia upanuzi wa nadharia hii ni pamoja na Lord Raglan (1936), katika kazi yake maarufu, *The Hero*. Yeye aliangalia visasili kwa kuhakiki mashujaa wa kitamaduni waliomo katika jamii za kilimwengu. Anasifika kwa kuibua motifu mbalimbali katika masimulizi ambapo alipata kuwa zilikuwa bia. Sifa moja kuu aliyoipata ni kuwa, motifu hizo zilikuwa na mfuatano maalum. Kwa mfano, kuzaliwa kwa shujaa kulitabiriwa, kutanguliwa kwa matukio maalum na ya ajabu kabla ya kuzaliwa kwa shujaa, jaribio la kuuliwa, kukimbilia nchi ya mbali kujisalimisha, kukabiliana na changamoto nyingi huko na hatimaye kurejea na kuikomboa jamii yake. Aidha, husalitiwa na mtu wa karibu naye na kufa kifo cha aibu. Wengine ni Propp ambaye alichunguza hurafa na kuangalia matukio katika kazi za kisanaa na visaasili.

### 1.8.2 Nadharia ya Naratolojia

Hii ni nadharia ya usimulizi. Kusimulia ni kueleza matukio kwa njia ya utendekaji wake yawe ya kubuni ama halisia. Kulingana na Genette (1980), nadharia ya usimulizi huelezea hali tatu ya usimulizi: kuelezea kauli ya kimaandishi ama kisimulizi iliyokusudiwa kuelezea tukio fulani (Wamitila 2002:139). Hii ina maana kuwa, mchunguzi huangalia dhamira ya msimuliaji katika matukio yanayoelezewa. Genette aidha anasema kuwa, naratolojia huchunguza mfuatano wa matukio katika kazi za kibunilizi ili kutambua kiini cha usimulizi husika na kubainisha maana. Genette vilevile anasema ya kwamba, nadharia hii hujihusisha na kuelezea tendo lenyewe la kusimulia katika kazi ya kifasihi na kama anavyoshadidia Wamitila (Wamitila 2002: 139).

Tunaweza kuelezea kauli za Genette kumaanisha ya kwamba, nadharia hii huchunguza masuala matatu katika usimuliaji ambayo ni: usimulizi, hadithi na tatu, usimuliaji. Usimulizi huhusu utambaji wa tukio. Yaani, namna mwandishi anavyoisuka hadithi yake. Hivi ni vitu viwili vinavyoingiliana na bila hivyo, kazi husika itakuwa chapwa. Hadithi kwa upande mwingine, ni matukio yaliyosimuliwa na mwandishi ama mtambaji. Huwa yamesukwa katika mfuatano wa kiwakati. Dhamira kuu ya naratolojia ni kuangalia sifa za simulizi na kuzidhihirisha na sifa

nyingine katika matini zinazochunguzwa. Nadharia hii huchukulia kuwa, kila usimulizi huwa na tabia fulani ama kuongozwa na kanuni fulani. Baadhi ya wahakiki wanasema kwamba, nadharia hii basi huangalia umuundo wa kazi husika. Swali kuu kwa wananaratolojia huwa ni, kazi husika ina mwelekeo gani?

Mojawapo wa mihimili muhimu ya nadharia hii ni kuwa, simulizi na hadithi huwasilishwa kwa njia mbalimbali na zilizotofautiana. Kwa mfano, msanii anaweza kufanya hivyo kwa kutumia ushairi ama riwaya kama huyu mwandishi ambaye tulichunguza kazi zake. Uchunguzi bora wa usimulizi basi ni sharti uonyeshe tofauti hizo. Nadharia hii inasisitiza kwamba, ni sharti mchunguzi kuhakiki kinachosimuliwa, matukio yenyewe pamoja na usimuliaji wenyewe na namna ulivyotekelezwa. Kwa njia hiyo, mhakiki ataonyesha kufanikiwa ama kutofanikiwa kwa msanii.

Mhimili mwingine ni kwamba, sio kila wakati matukio hufuatana kiwakati. Msanii huwa ameyakatiza kwa kutumia mbinu kama kisengere nyuma ama kisengere mbele kama njia ya kukumbusha ama kutabiri hatima ya matukio yanayosimuliwa. Katika masimulizi ya kinathari, aghalabu mtunzi hutoa maelezo halisi ya wahusika, mandhari na hata hali zao za kisaikolojia. Kupitia usimulizi wa aina hiyo, msomaji hupata hali halisi ya matukio na kutambua ni kwa nini mtunzi anasimulia kwa njia husika. Tukio likisimuliwa katika mfuatano wa kiwakati, msuko na pamoja na hadithi yenyewe huwa na mpangilio sawasawa. Yaani, msomaji anaweza kusema tukio la kwanza ni hili, la pili linafuatia hivi pamoja na yale mengine kwa mkumbo huo.

Pale ambapo matukio hayafuatani kwa kuzingatia kigezo cha wakati, hutokea mfuatano wa ki-*anakroni* (Wamitila 2002: 142). Mfuatono wa ki-anakroni hutumia mbinu ya kisengere nyuma na kisengere mbele. Kiona mbele huzungumzia matukio ambayo yatatokea baadaye-siku zijazo. Genette (1980), Rimmon-Kenan (1983) pamoja na Jahn (2005) wanakubaliana na kushadidia namna mbili za anakroni ambazo wanazitambua kama kisengere nyuma ama *analepsia* na kisengere mbele ama *prolepsia*. Kuna namna mbalimbali za kudhihirisha analepsia ama aina zake katika kazi za kifasihi kama tulivyobainisha katika kazi za mwandishi tuliyemhakiki.

Wakati ni kipengele muhimu katika simulizi yoyote. Ni katika wakati ambamo wahusika huishi, matukio hufanyika, na matendo ambayo ni kiini cha maudhui hutokea. Masuala yote katika simulizi huhusiana na hadithi kwa namna moja au

nyingine. Ni kwa sababu hii kipengele cha wakati kina nafasi muhimu katika simulizi inayokifanya kuhitaji kutafitiwa. Wakati hueleza ni lini ya hadithi. Vilevile hujibu suala la, 'kwa muda gani?' ama 'mara ngapi?'

Mbali na usimulizi wa kitabiri (kisengere mbele) na ule wa kisengere nyuma, kuna usimulizi mtawalia:  yaani matukio yanaimuliwa wakati uo huo. Kipengele hiki kinaibua dhana ya muda kulingana na nadharia hii. Dhana hii huibua masuala kama: tukio linachukua muda mrefu ama mfupi? Wananaratolojia hueleza hilo suala la muda kwa njia za vipengele vifuatavyo: muhtasari, udondoshaji, onyesho, uendelezaji, mvuto na idadi marudio. Muda wa matini huwa muhimu. Muda wa usomaji unatakiwa kuwa mfupi kuliko muda wa hadithi kulingana na nadharia hii. Muda wa hadithi huchangia kasi ya kisa kinachosimulia kwa njia ya muhtasari. Msanii hutoa kauli ya ufupisho kwa mfano kwa kutaja siku, miezi ama miaka ambayo tukio fulani lilichukua.

Njia nyingine ambayo hutumika ni udondoshaji. Maelezo fulani huwa yameachwa katika matini. Huwa kuna 'mwanadanungu' yaani, sufuri kwa sababu 'muda wa matini huwa ni mrefu kuliko muda-hadithi.' Nyakati mbili hizi huwa zinatofautiana kisimulizi. Dhana hiyo pia huibua kipengele cha uendelezaji. Katika uendelezaji, mtunzi ama msimulizi huegemea mawazo ya mhusika wa hadithini. Hili ni suala la saikolojia ama nafsi ya mhusika. Hali hiyo ndiyo huleta suala la mvuto katika usimulizi.

Kuhusu urudiaji, nadharia ya naratolojia hulieleza kwa njia kadhaa. Hujihusisha na ni mara ngapi tukio fulani hurudiwa katika matini. Hali hiyo huonyesha umuhimu wa tukio linalosimuliwa. Kurudiwarudiwa huko aghalabu huwa sio kamilifu na hutegemea masuala kama muktadha. Kurudiwa mara nyingi aidha huonyesha matokeo ya tukio linalorejelewa kwa mkondo wa hadithi na hatima ya mhusika ama hali husika.

Baadhi ya mihimili ya nadharia hii tuliyopata ni kuwa:

1. Wahusika ni kipengele muhimu cha usimulizi. Hii ni kwa sababu, mwandishi anaweza kutoa maelezo kumhusu mhusika fulani ambayo hutusaidia kumwelewa kisaikolojia na mchango wake kwa tukio linalosimuliwa. Njia nyingine huwa ni kuangalia matendo ya wahusika, maumbile na mazingira

ambamo wanapatikana. Hali hizo na nyingine kama mandhari na hali zao huchangia kubainisha dhima ya tukio wanalolikuza.

2. Mhimili mwingine muhimu wa nadharia hii ni mtazamo wa msimulizi kuhusu kisa ama matini anayoyasimulia. Lengo la mtunzi yeyote huwa ni kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira yake. Hali hiyo ndio huonyesha mtazamo wake kuhusu masuala mbalimbali anayoyasimulia. Mhakiki anaweza kukadiria ni masuala gani anaunga mkono ama anayakashifu katika jamii ya uandishi.
3. Nadharia ya naratolojia pia hutilia maanani suala la wakati wa kusimulia. Kila tukio hutendeka katika wakati maalum. Nadharia hii basi hujishughulisha na kuangalia 'wakati –hadithi' na 'wakati-matini.' Dhana ya wakati-hadithi huhusu muda ambao hadithi inachukua kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kisa. Inaweza kuwa siku, miezi ama miaka. Wakati-matini hurejelea muda ambao kazi fulani inachukua kusomwa na msomaji fulani. Hili ni suala la mtu binafsi kwani kila mtu ana uwezo tofauti wa kusoma ama kasi. Hata hivyo, vipengele hivi viwili huhusiana wakati mwingine katika masimulizi. Katika utafiti wetu, tulitumia mihimili yote minne tuliyoitambua kutokana na nadharia hii kwa kuangalia namna ambayo mtunzi M.S. Abdulla alivyoishughulikia katika kazi yake.

Hii ndio mihimili ya nadharia hii ambayo tuliitumia katika kazi yetu wakati wa kuchanganua data katika utafiti huu.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji ulikusanyaji data kutoka katika vitabu teule kwa njia ya kusoma na kuandika. Mbinu hizi zilihitajika ili kutambua aina ya vifaa na kutambua aina ya sampuli ambayo tulihitaji kuihoji (Tromp na Kombo 2006). Baadaye, uchanganuzi wa data uliwasilishawa na matokeo kulingana na malengo ya utafiti wetu. Malengo ya utafiti huu yalikuwa yafuatayo: kudhihirisha aina za misuko katika riwaya teule za M. S. Abdulla, kudhihirisha aina ya usimulizi anaoutumia M. S Abdulla katika riwaya zake teule pamoja na kuonyesha kunga za lugha katika riwaya zilizoteuliwa.

#### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Data ya kimsingi ilipatikana kwa kusoma vitabu teule kwa kuzingatia malengo ya utafiti wetu na kwa kuongozwa na nadharia ya Umitindo. Vitabu teule ambavyo

tulisoma ni: *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.* Awali, tulikuwa tumesoma kutoka maktabani tasnifu, majarida, vitabu, makala pamoja na matini mbalimbali kuhusu mwandishi huyu na kazi zake mbalimbali.

### 1.9.2 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo

Baada ya kupata data, tuliichanganua kwa kwa kutumia malengo, maswali na nadharia ya umtindo. Hatimaye tuliwasilisha matokeo katika sura zifuatazo:

Sura ya Kwanza: Msingi wa utafiti,

Sura ya Pili: Msuko katika kazi *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007)

Sura ya Tatu: Usimulizi katika kazi teule za M. S. Abdulla.

Sura ya Nne: Matumizi maalum ya kunga za lugha katika kazi teule za M. S. Abdulla.

Sura ya Tano: Matokeo na Mapendekezo ya Utafiti.

# SURA YA PILI

# MSUKO KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007)

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia msingi wa utafiti. Katika Sura ya Pili tulishughulikia lengo la kwanza la utafiti wetu. Lengo la kwanza lilihusu kuchunguza aina za misuko ambayo mwandishi M. S. Abdulla alitumia katika riwaya zake za: *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.*

## 2.1 Aina za Misuko

Kulingana na Gennette (1980), nadharia ya usimulizi huelezea hali tatu za usimulizi katika kuelezea kauli ya kimaandishi ama kisimulizi iliyokusudiwa kuelezea tukio fulani (Wamitila 2002:139). Hii ina maana kuwa, mchunguzi huangalia dhamira ya msimuliaji katika matukio yanayoelezewa. Genette aidha anasema kuwa, naratolojia huchunguza mfuatano wa matukio katika katika kazi za kibunilizi ili kutambua kiini cha usimulizi husika na kubainisha maana. Gennette vilevile anasema ya kwamba, nadharia hii hujihusisha na kuelezea tendo lenyewe la kusimulia katika kazi ya kifasihi na kama anavyoshadidia Wamitila (2002: 139). Tunaweza kuelezea kauli za Genette kumaanisha ya kwamba, nadharia hii huchunguza masuala matatu katika usimuliaji ambayo ni: usimulizi, hadithi na tatu, usimuliaji. Usimulizi huhusu utambaji wa tukio. Yaani, namna mwandishi anavyoisuka hadithi yake. Hivi ni vitu viwili vinavyoingiliana na bila hivyo, kazi husika itakuwa chapwa. Hadithi kwa upande mwingine, ni matukio yaliyosimuliwa na mwandishi ama mtambaji. Huwa yamesukwa katika mfuatano wa kiwakati.  Dhamira kuu ya natarolojia ni kuangalia sifa za simulizi na kuzidhihirisha na sifa nyingine katika matini zinazochunguzwa. Nadharia hii huchukulia kuwa, kila usimulizi huwa na tabia fulani ama kuongozwa na kanuni fulani. Baadhi ya wahakiki wanasema kwamba, nadharia hii basi huangalia umuundo wa kazi husika. Swali kuu kwa wananaratolojia huwa ni, kazi husika ina mwelekeo gani? Swali hili limevutia majibu kutoka kwa wataalamu mbali mbali wakiwemo Msokile, Senkoro na wengineo.

Msuko hutumiwa kueleza mtiririko wa vitushi na matukio katika kazi ya fasihi (Msokile 1993:3). Msuko hutumiwa na wahakiki wa kifasihi kuchunguza mfuatano wa matukio yanayopatikana katika kazi iliyoandikwa na jinsi inavyochangia namna

maudhui yanakuzwa. Katika kushughulikia matukio, mchunguzi huangalia jinsi tukio moja husababishwa na tukio jingine (Wamitila, 2006). Hii ndio sababu mhakiki wa kazi za kifasihi huwa anajiuliza maswali kama: matukio husika yanasababishwa na nini? Yanatukia hivyo kwa sababu gani? Matokeo yake ni gani? Katika kuchunguza kipengele cha msuko, lazima mhakiki ajiulize ni kwa nini tukio fulani linatokea mwanzo na ni kwa nini tukio fulani limetanguliwa na tukio lingine? Kwa hivyo, msomaji wa matini za kifasihi ni sharti achunguze jinsi mwandishi alivyosuka kazi yake na kuunganisha matukio kuanzia tukio la kwanza hadi tukio la mwisho.

Msuko unahusiana na usimulizi. Kulingana na Senkoro, misuko huwa sio ya ya aina moja pekee (Senkoro 1976). Yeye anaainisha misuko ifuatayo: msuko msago, msuko kioo, msuko mwisho-kati-mwanzo, msuko mwanzo-kipeo na msuko rudufu. Katika msuko sahili, wahusika, vitushi na matukio huwa yanasimuliwa kwa njia ya mantiki. Kulingana na msuko wa aina hii, matukio huwa yanayotiririka kuanzia mwanzo hadi tukio la mwisho kwa njia ya mfululizo (Oyoyo, 2013:13). Msuko sahili huonyesha namna matukio yanavyofuatana kimpangilio na kumpa msomaji wa kifasihi nafasi ya kuyafuatilia kikamilifu. Kazi zinazohakikiwa katika utafiti huu zilidhihirisha misuko mbalimbali. Katika riwaya za; *Kisima cha Giningi (1968)* na *Kosa la Bwana Msa* (2007), tulishughulikia aina tatu za misuko: msuko sahili, msuko kioo na msuko mwanzo-kipeo kulingana na lengo la kwanza la utafiti wetu.

### 2.1.1 Matumizi ya ki-Anakroni

Mhimili mojawapo wa nadharia ya naratolojia ni kwamba, sio kila wakati matukio hufuatana kiwakati. Msanii huwa ameyakatiza kwa kutumia mbinu kama kisengere nyuma ama kisengerembele kama njia ya kukumbusha ama kutabiri hatima ya matukio yanayosimuliwa. Katika masimulizi ya kinathari, aghalabu mtunzi hutoa maelezo halisi ya wahusika, mandhari na hata hali zao za kijisaikolojia. Kupitia usimulizi wa aina hiyo, msomaji hupata hali halisi ya matukio na kutambua ni kwa nini mtunzi anasimulia kwa njia husika. Tukio likisimuliwa katika mfuatano wa kiwakati, msuko na pamoja na hadithi yenyewe huwa na mpangilio sawasawa. Yaani, msomaji anaweza kusema tukio la kwanza ni hili, la pili linafuatia hivi pamoja na yale mengine kwa mkumbo huo.

Katika msuko sahili, matukio yote katika kazi za kifasihi hufuatana bila kutumia mbinu kama rejeshi. Hufanya hivyo ili kuondoa utata katika kazi husika. Msuko

sahili, hutiririka kwa njia ya A-B-C-D kama anavyoshadidia (Wamitila 2010:41). Matukio hayo hufuatana kutoka tukio la kwanza hadi la mwisho kimpangilio. Matukio yanayosimuliwa huwa yanajengana na kukamilishana. Vitushi pia huwa vinajengana kimoja baada ya kingine. Misuko hiyo ilijidhihirisha kikamilifu katika kazi tulizozihakiki za mwandishi huyu. Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa,* matukio yanafuatatana vifuatavyo:

> Eh! Nasikia mlio wa gari linakuja! Haiwezi kuwa Bw. Ali. Katika barua yake Bw. Ali kasema atakuja kesho-kutwa asubuhi mapema kama hivi labda. Lakini nani huyo, basi?.. Mgeni wetu nini, bibi? Aliuliza Jamila kwa adabu na maungwana. “Karibu ndani.”
>
> Bibi yule alisimama tutwe, anamtazama tu, halafu tena “Unasema karibu ndani, na wewe umesimama mlangoni-nitapita wapi basi, mimi? Adabu kishamba namna peke yake. (uk.7) “…Sasa wewe ndicho kidimu cha shamba aliyeninyang’anya mume wangu? Naam, umesemaje, bibi? Jamila alitekewa akatunduwaa. Umesikia!” alijibu yule bibi kwa jeuri. Nakuuliza wewe ndiye mbuya wa mume wangu? (uk. 8)

Kulingana na dondoo, Jamila alikuwa hana uhakika ya kuwa, mumewe Bwana Ali ndiye alikuwa anarejea nyumbani siku hiyo. Katika barua aliyoisoma, mumewe alikuwa amemweleza ya kwamba, angerejea nyumbani kesho kutwa asubuhi na mapema na wala sio siku hiyo. Jamila kisha anamkaribisha bibi mmoja aliyeshuka kutoka garini. Kulingana na nadharia ya umtindo, kazi tofauti za waandishi tofauti zinaweza kutofautishwa katika misingi ya sifa za kimitindo zilizotumika katika kazi husika. Lengo la mwandishi na maswala ambayo anataka kuyaibua ndiyo humuamulia mtindo atakaoutumia (Senkoro 1988:6). Kwa mujibu wa msuko wa aina hii, vitushi hupangwa kwa ufundi mkubwa sana ili kukuza masimulizi. Ilidhihirika ya kuwa, masimulizi haya yamepangwa kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho. Pale ambapo matukio hayafuatani kwa kuzingatia kigezo cha wakati, hutokea mfuatano wa ki-*anakroni* (Wamitila 2002: 142). Mfuatono wa ki-anakroni hutumia mbinu ya kisengerenyuma na kisengerembele. Kiona mbele huzungumzia matukio ambayo yatatokea baadaye-siku zijazo. Genette (1980), Rimmon-Kenan (1983) pamoja na Jahn (2005) wanajadili namna mbili za anakroni ambazo wanazitambua kama kisengere nyuma ama *analepsia* na kisengere mbele/ ama *prolepsia*. Kuna namna mbalimbali za kudhihirisha anaplesia ama aina zake katika kazi za kifasihi kama tulivyobainisha katika kazi za mwandishi tuliyemhakiki.

Tukio A-linaanzia pale ambapo ni njiani ambapo Jamila anatoka posta hadi B-anapofika kizingitini mwake na jinsi watumishi wake wanavyompokea. Tukio C – ni jinsi ambavyo bibi yule anavyokuja na kujitoma ukumbini mwake na kisha kuzua fujo. Tukio D – ni pale ambapo anamwonya na kumtahadharisha kuwa, mumewe akija tena kwa Jamila, basi hatafika salama kwani ataaga dunia kabla ya kufika huko. Aina hii ya msuko humwezesha msomaji kupata mfululizo wa vitushi haraka na ufuatilizi huwa mwepesi riwaya za *Kosa la Bwana Msa* na *Kisima cha Giningi.* Mlacha na Madumulla wanasema ya kwamba, msuko wa aina hii hutumiwa sana katika kazi za kipelelezi. Hii ni kwa sababu riwaya hizo huchukua mara nyingi zinahusisha masuala ambayo jamii huhusiana nayo kwa njia ya ukaribu sana (Mlacha na Madumulla 1991:58-60).

Katika Sura ya Sita, mwandishi anaeleza:

> Alipofika mlangoni, aliufungua taratibu asije akamwamsha bibi yake. Kutazama ndani aliona chumba kitupu, utupu wa chumba ulimnyarisha ukamzomea kimya kimya! Safinia hakujua afanye nini, afikiri nini. Alitoka mbio, na maziwa yalimtikisa kifuani kufuatisha mwendo wa haraka, mpaka alikokuwako Siajabu. Na macho kayatoa, alimpigia kelele mjoli wake kama yuko mbali, mtu yuko mbele yake, Siajabu! Mtoto hayumo chumbani mwake-la yeye wala bwana mdogo! Unasemaje? (uk. 23)

Katika dondoo hili, mwandishi anasimulia jinsi Safinia anamtafuta Jamila ili apate ushauri. Baadaye anaelekea kwa Siajabu na kumweleza alichokiona. Tukio linalofuatia ni lile la kumtafuta Jamila hadi msalani. Inabainika kwamba, Jamila hayupo ila ameenda hospitalini mjini kuchukua dawa za mgonjwa wake na wangemtarajia kesho yake. Masimulizi haya mafupi yamepangwa kwa njia ya moja kwa moja kutoka tukio moja hadi jingine. Huu basi ni msuko sahili. Kulingana na nadharia ya umtindo, athari ya kusimulia hivyo ni kuwa, msomaji wa riwaya hii anaweza kufuatilia matukio ya kitabuni moja kwa moja bila kukanganyika na kuelewa maudhui kwa njia ya uwazi zaidi. Kulingana na nadharia ya umtindo, katika aina hii ya msuko, wahusika, vitushi na matukio yanasimuliwa kwa njia ya mfuatano kimaantiki (Wamitila 2010:41). Mbinu hii basi inamfanya msomaji wa riwaya hii kuing'amua dhamira ya kazi kwa wepesi.

Wakati ni kipengele muhimu katika simulizi yoyote. Ni katika wakati ambamo wahusika huishi, matukio hufanyika, na matendo ambayo ni kiini cha maudhui

hutokea. Masuala yote katika simulizi huhusiana na hadithi kwa namna moja au nyingine. Ni kwa sababu hii kipengele cha wakati kina nafasi muhimu katika simulizi inayokifanya kuhitaji kutafitiwa. Wakati hueleza ni lini ya hadithi. Vilevile hujibu suala la, 'kwa muda gani?' ama na 'mara ngapi?' Msuko sahili pia unapatikana katika riwaya ya, *Kosa la Bwana Msa*. Tunanukuu:

> Basi mfike nyumbani leo wakati wa saa kumi; bibi ana kazi yake muhimu na ya haraka sana, anataka kukupeni. Lakini mje kwa siri sana kama mlivyofanya safari ile; mjaribu kama itakavyokuwa asikuoneni mtu! La, kwa kuingia wala kwa kutoka. Piteni kule kichochoroni kwenye kilango kilichoko ubavuni mwa nyumba yetu. Mnasikia hivyo? (uk. 33)

Katika dondoo hili matukio haya yanatukia katika duka maarufu linalojulikana kama 'Kwa Mramu'. Duka hili lina sifa ya kujaa na kutoondoka watu mchana kutwa na katika sehemu ya usiku. Shoka na Joka wanatakiwa kwenda Forodhani saa kumi kwa sababu kuna kazi iliyokuwa ikiwangoja. Wanapewa nauli ila wanakwenda kunywa pombe kama tukio la kusubiri muda wa kutekeleza uhalifu wao. Kupitia mbinu hii tunabainisha ya kwamba, pombe inatumiwa na mwandishi kama kidhibiti cha matendo ya wahusika katika riwaya teule. Hali kama hiyo inajirejelewa katika (uk. 36). Tunaelezwa, "Nakupeni ujira wenu kabisa; mkisha kazi yenu, hamna haja ya kuonana na mimi tena, mpaka initokezee kazi nyingine nikwiteni." Kisha wahusika wanapewa pesa zao kwa hasira na Bi. Shinuna na kisha anawafukuza. Hilo lilikuwa tukio la kihalifu. Wahusika hawa walitakiwa kulizuia gari kwa niaba ya Bi. Shinuna. Bi. Shinuna anawaeleza kwamba kazi watakayoifanya ni kulizuia gari lenye rangi ya maziwa wakati wa alfajiri. Kwa kuwa uhalifu ulikuwa utekelezwe katika kipindi maalum, mwandishi anaibua msuko mwingine (kunywa pombe) ili kuwadhibiti wahusika badala ya kusimulia zaidi. Matukio haya yanatiririka moja kwa moja na kubainisha dhamira ya mhusika Shinuna.

Matukio ya msuko sahili huondoa uwezekano wa kuwachosha wasomaji wa kazi za kifasihi. Mwandishi huyu ameutumia msuko wa aina hii kwa lengo kuepuka masimulizi marefu ambayo yangemchosha msomaji. Mwandishi huyu basi anadhihirisha dhana kwamba, msuko mwafaka ni pale ambapo msomaji wa kazi ya kifasihi anaweza kutabiri kila tukio na kwa hivyo kuyafanya masimulizi ama matukio yasisimue. Hali sawia na hiyo inajitokeza katika Sura ya Kumi na Moja, katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa.* Tunaelezwa:

> …kisha wanaume wakaondoka wakajitanibu na wanawake kwa kwenda faraghani huko sebuleni kwenda kuvuta sigara. Walikaa ubavu kwa ubavu juu ya kochi, wakawasha sigara zao, wakawa wanavuta… Yahe Manulla, Alizuka Aziz kwa ghafla (uk. 55)

Masimulizi yote haya yahahusu mazungumzo kati ya Aziz Akram na Amanulla pembezoni ambapo wanakaa faraghani huku wakivuta sigara. Mazungumzo yao wanayaelekeza kwa Jamila. Akram anataka kumposa Jamila haraka iwezekanavyo na hata kufanya harusi haraka haraka na kimya kimya. Amanulla anatilia shaka jambo hili japo anamwahidi kwamba atajaribu kumshawishi Jamila. Jamila na Aziz Akram wanaelekea Dubai. Matukio haya yanaanza na **A** ambapo mapochopocho ya mgeni yanaandaliwa hadi **B**, ambapo Aziz Akram anapofika na kukaribishwa na kisha **C** ambapo wanapozama katika mazungumzo yao na mwisho **D** ambapo Aziz na Amanulla wanapoenda faraghani. Mazungumzo haya yameendelezwa kupitia msuko sahili. Msuko wa aina hii aidha unajibainisha katika sura ya Kumi na Mbili pia (uk. 61).

Katika ukurasa husika, ni Forodhani, nyumbani kwa Bi. Shinuna na mumewe Ahmed bin Soud. Ahmed ameshikilia kwamba, lazima asafiri siku hiyo wala hawezi katu kuihairisha safari ya kwenda Nairobi katika shughuli za kikazi. Bi. Shinuna alifahamu vyema kuwa Bwana Ali haendi Nairobi kwa shughuli za kikazi ila anakwenda Chwaka kumwona Jamila. Tukio hili linadokeza jinsi Bwana Msa na Spekta Seif wanalikaribia gari la Bw. Ali na kumwambia asiwe na hofu na kumhakikishia usalama wake. Joka na Shoka wanapoliona gari lenye rangi ya maziwa nao walitia gari lao moto na kuanza kuwafuata. Matukio yanadhihirisha jinsi mwandishi M. S. Abdulla amedhihirisha utumizi wa msuko sahili kwa kiwango kikubwa katika riwaya hizi teule. **A**, mandhari ni Forodhani Bw. Ali akitofautiana na mkewe Bi. Shinuna kuhusu safari yake. **B**, Bw. Ali akiwa njiani huku amefuatwa unyo kwa unyo. **C**, njiani ambapo gari lake linasimama huku Shoka na Joka wakisukasuka mapanga yao na wakimjia na mwisho pale ambapo manunda hawa wiwili Shoka na Joka, wanaandamana na askari kwenda kwenye gari la polisi. Wanalifuata gari la Bwana Ali kwa mwendo ule ule aliokuwa nao. Wanafukuzana na kufikia gogo la mti barabarani. Gari la Ahmed linasimama ghafla kisha Shoka na rafikiye Joka wanatokea ghafla huku wakisukasuka mapanga yao hewani tayari kumvamia Bwana Ali.

Msuko katika tukio hili ni sahili kwani matukio yanafuatana moja kwa moja katika sura zilizotajwa. Aidha misuko yote haina mbinu rejeshi ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza. Matukio ya msuko sahili kulingana na nadharia ya naratolojia huondoa uwezekano wa kuwachosha wasomaji katika usimulizi kama anavyoshadidia Oyoyo (2013). Vile vile msuko huu kupitia nadharia ya naratolojia ni mwafaka kwani wasomaji wanaweza kutabiri kila tukio na kwa hivyo, kuyafanya masimulizi ama matukio yasisimue.

Mbali na usimulizi wa kitabiri (kisengerembele) na ule wa ki-kisengerenyuma, kuna usimulizi mtawalia:  yaani matukio yanasimuliwa wakati uo huo. Kipengele hiki kinaibua dhana ya muda kulingana na nadharia hii. Dhana hii huibua masuala kama: tukio linachukua muda mrefu ama mfupi? Wananaratolojia hueleza hilo suala la muda kwa njia za vipengele vifuatavyo: muhtasari, udondoshaji, onyesho, uendelezaji, mvuto na idadimarudio. Muda wa matini huwa muhimu. Muda wa usomaji unatakiwa kuwa mfupi kuliko muda wa hadithi kulingana na nadharia hii. Katika *Kisima cha Giningi*, msuko sahili umejitokeza katika Sura ya Tatu hadi Sura ya Tano. Tunaelezwa:

> Hapa, Spekta, lazima awe kaja mtu mwingine aliye na kinyume na mume wa huyu bibi kwa mengi. Moja katika hayo inataka awe mfupi wa kimo, tena awe na tamaa kubwa kuliko mumewe huyu bibi ambaye haja yake kama itakavyokuwa, ni pesa tu za matumizi wala si utajiri wa kuwa na visanduku vya mapauni. (uk. 32)

Matukio yote yanaendelezwa kwa msuko sahili. Mandhari ya Sura ya Tatu ni chumbani kwa Mwana wa Giningi. Spekta Seif na Bwana Msa wamefika kwa Mwana wa Giningi ili kupeleleza kisa cha wizi baada ya Mwana wa Giningi kuona ugeni wa kipande cha sigareti aina ya chapa ya *Cent*, ufunguo wa sanduku pamoja na msahafu mkuukuu mezani badala ya mahali pake pa kawaida kwenye rafu. Msuko sahili una mchango mkubwa kwa msomaji wa kawaida wa kifasihi kwa sababu unamwezesha msomaji kufuatilia matukio moja kwa moja bila kutatizika. Pili, matukio yamepangwa kimpangilio kwa njia ya moja kwa moja na ni rahisi kutambua maudhui kwa wepesi. Dondoo hili linahusu namna ya kupata ushahidi baina ya Bwana Msa na Spekta Seif kuhusu mwizi aliyesambaratisha chumba cha Mwana wa Giningi. Spekta Seif anamshuku mume wa Mwana wa Giningi ilhali Bw Msa anakana kuwa siye na lazima awepo mtu mwingine aliyekuja pale. Sajin Paolo anatumwa kumkamata Vuai

kisha Spekta Seif na Bw Ali wanaenda kwa Ali Makame-babake mdogo Mwana wa Giningi. Hata hivyo, Vuai hayuko nyumbani kwake. Safari yao basi inawaelekeza kwa Fundi Mangungu. Matukio hayo yanaonyesha namna maudhui ya ushirikina yanavyotumiwa na wahusika kutekeleza uhalifu na pia kuuficha. Bw Msa anapofika kwa Fundi Mangungu, mganga huyu anamweleza Bw Msa kuwa ampe shilingi mbili za uganga. Kunaibuka ubishi kati yao. Kupitia msuko huu, Bw Msa anamsaidia msomaji kugundua kuwa waganga ni wadanganyifu na hawajui kitu. Hali kama hiyo inashuhudiwa katika Sura ya Nane ya riwaya ya *Kisima cha Giningi*.

Katika sura hiyo, mwandishi anaoonyesha maficho ya wahalifu. Walitumia mandhari ya chini ya *Kisima cha Giningi* kujificha na kuficha mali ya wizi. Hapa, tunawaona wezi wakiwa wameiba, na wezi wakiiba. Msuko husababisha matukio kusababishana na kutegemeana kwa njia ya kisengerenyuma. Katika riwaya ya, *Kisima cha Giningi,* tunasoma ya kuwa, Spekta Seif, Bw Msa, Sajin Paolo na askari wawili wapo katika kisima hiki kuchunguza kifo cha Mwana wa Giningi. Maiti ya Mwana wa Giningi ina jeraha la kisu kifuani ambalo lilifika hadi ndani ya moyo, pua ilikuwa imekatwa kipande na mkono wake wa kushoto ulikuwa umechongwa kama mkono wa kulia. Watu waliokuwepo pale kisimani na kuhojiwa wanaelekea kumtuhumu Vuai kwa mauaji ya Mwana wa Giningi. Hii ni kwa sababu, tukio lililotangulia linaashiria hali inayomtuhumu Vuai. Mwana wa Giningi alipokuja kuteka maji kisimani, ugomvi ulizuka kati yao na wakaandamana wote kisimani lakini wakati wa kurudi Mwana wa Giningi hakuonekana ila Vuai, mumewe. Kulingana na nadharia ya Umtindo, uchunguzi wowote unaohusisha msuko kwa hivyo ni lazima uchunguze visababishi vya tukio la sasa. Mwandishi anatumia tukio hilo kubainisha udhaifu wa asasi ya ya polisi ilivyopungukiwa katika kukabiliana na uhalifu katika jamii ya Giningi. Vuai anashikwa kwa kudhaniwa ndiye mhalifu kimakosa. Hali hiyo hata hivyo inabatilishwa na tukio linalofuatia wakati Bw Msa anasisitiza kuingia katika vyumba vya ndani katika kisima. Katika riwaya, tunaelezwa ya kuwa wahalifu walitupa kitu chenye rangi nyeusi na ingawa mhalifu alitaka kukiokota, alihofia kukamatwa na kwa hivyo akakiacha nyuma (uk. 87).

Hili ni tukio ambalo linaonyesha juhudi zinazofanywa na asasi ya polisi kukabiliana na uhalifu katika jamii ya Giningi wanapokuwa na ari ya kufanya hivyo. Mwandishi alitumia tukio hili kusisitiza ushirikiano baina ya umma na asasi ya polisi kama njia

ya kukabiliana na uhalifu katika jamii hii. Haya ni matukio ambayo yanamsaidia msomaji kutambua kiini cha uhalifu na pale ambapo wahalifu wanajificha na kuficha mali waliyoiba. Masimulizi haya katika *Kisima cha Giningi* kuanzia Sura ya Nane hadi Sura ya Kumi yanaendelezwa kupitia msuko sahili wa moja kwa moja ambao ni nadra sana kumtatiza msomaji yeyote. Ni msuko ambao ulifanya usomaji wa riwaya husika kuwa wa kuvutia na rahisi kuelewa.

### 2.1.2 Msuko Kioo katika Riwaya Teule

Msuko kioo husimuliwa matukio kutoka mwanzo kwa kutumia kanuni na taratibu za miundo mingine kama vile msuko msago, mwanzo-kati, kati-mwisho au mwisho-mwanzo (Muhando na Balisidya 1976:3). Hata hivyo, katika usimulizi wa aina hii, msuko wa aina hii husimulia matukio kwa kurudia jambo lililokwisha kuelezwa hapo mwanzo. Yaani, aina hii ya msuko hutumia mbinu rejeshi kwa wingi ili kueleza uhusiano uliopo baina ya tukio la sasa na lililotangulia. Kulingana na nadharia ya naratolojia, pale ambapo matukio hayafuatani kwa kuzingatia kigezo cha wakati, hutokea mfuatano wa ki-*anakroni* (Wamitila 2002: 142). Mfuatono wa ki-anakroni hutumia mbinu ya kisengerenyuma na kisengerembele. Kiona mbele huzungumzia matukio ambayo yatatokea baadaye-siku zijazo. Genette (1980), Rimmon-Kenan (1983) pamoja na Jahn (2005) wanashadidia namna mbili za anakroni ambazo wanazitambua kama kisengere nyuma ama *analepsia* na kisengere mbele ama *prolepsia*. Kuna namna mbalimbali za kudhihirisha anaplesia ama aina zake katika kazi za kifasihi kama tulivyobainisha katika kazi za mwandishi tuliyemhakiki.
Pia, huweza kuwa na athari ya kuibua maana na mantiki ya hali ya sasa. Aina hii ya msuko vilevile huwa ni matukio ya kudakizana ijapo matukio huwa yanakamilishana kutokana na njia za kifasaha ambazo mtunzi anatumia. Msuko kioo hutumia mbinu ya kisengere nyuma na viona mbele kwa wingi (Senkoro, 1982).

Katika *Kosa la Bwana Msa*, msuko wa a kioo unajitokeza katika Sura ya Kwanza, pale ambapo mtumishi wa Bi Shinuna, Tunu anamweleza Bi. Shinuna kuwa mume wake Bwana Mdogo ameweka maskani kule Chwaka ambako amekodisha nyumba. Tunaelezwa:

> Haiwezekani kuwa! Kabisa haiwezi kuwa! Tunu sasa, unajifundisha kuzua wewe, unasema bwana wako! Vipi Ahmed aniache mimi hapa aende akakae na kidimu huko shamba, na-kwa namna unavyosema wewe- katika nyumba nzuri, yenye

> bustani ya miwaridi na miasimini? Jambo hilo, Tunu, ni muhali; haliingii akilini hata kidogo. (uk. 3)

Katika usimulizi wa aina hii, mwandishi wa fasihi hutumia aina ya msuko kusimulia matukio kwa kurudia jambo lililokwisha kuelezwa hapo mwanzo. Ni msuko ambao hutumia mbinu rejeshi kwa wingi ili kueleza uhusiano uliopo baina ya tukio la sasa na lililotangulia. Inadhihirika waziwazi pia kuwa Bi. Shinuna alikuwa gizani hadi pale Tunu alipomfichulia siri. Masimulizi haya ambapo Tunu anamweleza Bi. Shinuna kuwa analiwa kivuli yameendelezwa kupitia kisengere nyuma. Kisa hiki ndicho kisababishi cha Bi. Shinuna kwenda kule Chwaka kumkaripia Jamila. Tunu anamweleza Bi. Shinuna kuwa alifanya upelelezi wake na ameambiwa kuwa nyumba ile aliyokodisha amemweka mke fulani. Anamweleza pia kuwa alifanya uchunguzi wake zaidi na akamwona mke aliyekodishiwa nyumba. Msuko kioo una athari kubwa kwa msomaji wa riwaya hizi teule kwa sababu japo tunaelezwa matukio yaliyoelezwa hapo mbeleni, matukio hayo yanasisitizwa na kuelezwa kwa undani ili msomaji aweze kuelewa ipasavyo.

Kuhusu urudiaji, nadharia ya naratolojia hulieleza kwa njia kadhaa. Hujihusisha na ni mara ngapi tukio fulani hurudiwa katika matini? Hali hiyo huonyesha umuhimu wa tukio linalosimuliwa. Kurudiwarudiwa huko aghalabu huwa sio kamilifu na hutegemea masuala kama muktadha. Kurudiwa mara nyingi aidha huonyesha matokeo ya tukio linalorejelewa kwa mkondo wa hadithi na hatima ya mhusika ama hali husika. Katika ukurasa wa 8 hadi 9 tunamwona Bi. Shinuna anajitoma ukumbini na macho yake yanatua kwenye picha iliyo ukutani. Anadai kwamba Jamila amemnyang’anya muwewe. Bi. Shinuna anamtahadharisha na kumwonya kwamba, asipoachana na mumewe basi atamdhuru. Tunaelezwa kuhusu Mwanatenga na uhusiano wake na Jamila. Mwandishi Abdulla anasema kuwa Mwanatenga alikuwa shogake waliyesoma naye katika shule ya Dahiliya iliyokuwapo hapo Forodhani. Mwanatenga alikuwa mkaazi wa Makunduchi. Baba yake alikuwa tajiri na alisikia kwamba katika miaka ya hivi karibuni, rafiki yake naye aliishi kule Vuga ambapo alikuwa ameolewa vilevile na mume tajiri. Mawazo haya ya msimulizi ndicho kisababishi cha Jamila kutoroka kwake Chwaka na kuhamia kwa rafiki yake ambaye walijuana walipokuwa shuleni aliyeitwa Mwanatenga. Katika ukurasa wa 13, tunaambia kuwa, Jamila alitembelea kituo cha basi kama saa kumi na mbili na nusu

akisindikizwa na mtoto wake kwa jina Soud. Walikuwa pia na mzigo. Katika sura ya 7, yafatayo yanajitokeza:

> Nilimwuliza Sheha kama kipo kitu kilichopotea ndani yake, akasema hakuna kilichopotea. Nini basi dhamiri ya kukichukua huko kikawekwa juu ya meza? Kutazama mimi kwa uangalifu karatasi moja, niliona kuwa moja imechanwa kwa uangalifu kabisa, hata mtu hawezi kujua kama pale pamechanwa karatasi. Sheha alistaajabu nilipomwambia, akawa anaona taabu kumtuhumu Jamila kuwa ndiye aliyetenda tendo lile; kwa hakika alimkatalia Jamila katakata kuwa Jamila hafanyi hivyo. (uk. 28)

Kupitia dondoo, ilibainika jinsi Sheha alivyomwamini Jamila. Hata anapoambiwa na Bw Msa kuwa alidhani kwamba Jamila ndiye aliyetenda kitendo kile, ilikuwa vigumu kwa Sheha kukubali. Kisa hiki kimesimuliwa kupitia msuko kioo na hasa ndicho kisababishi cha Sheha Judi kwenda kumwona Jamila kwake nyumbani. Kule ndiko alikokutana na Bi Safinia akamwambia kwamba hayupo ila ameenda hospitalini mjini kuchukua dawa za mgonjwa wake na wangemtarajia kesho yake. Juhudi za Sheha Judi hazikufua dafu. Mwishowe, Safinia alimwamuru atoke nje kisha anaufunga mlango kwa kitasa na kumuaga. Japo tumeelezwa kuhusu kadhia ya Jamila na kilichompata Chwaka na hata kilichofanyika alipoenda kwa Shehe Judi, hadi akapanga safari ya kwenda Vuga kwa Mwanatenga. Tunarejeshwa nyuma na kuelezwa tena katika Sura ya Tisa (uk. wa 38). Wakati mumewe anaporejea kutoka karamu ya jamaa yake, Seyyid Ahmed bin Soud, anamsimulia kisa cha shogake walipokuwa peke yao. Tunaambiwa kuwa alimwambia Amanulla kama alivyosimuliwa na Bwana Msa aliyemleta. Mwanatenga alimsimulia mume wake masuala mengi kumhusu Jamila na matukio yaliyompata huko Chwaka hadi kufikia kupelekwa nyumbani kwao kwa msaada wa Bw Msa. "Mradi, Mwanatenga hakubakisha hata lapata hivi, tangu ya shamba, sababu ya kukimbia shamba na kufikishwa kwao". (uk. 38). Tunaona jinsi mwandishi anavyoendeleza msuko kioo kwa kusisitiza kadhia aliyokumbana nayo Jamila. Aina hiyo ya msuko inatiwa matukio katika riwaya wazi na kwa njia ya uwazi zaidi kwa msomaji.

Lengo la mtunzi yeyote huwa ni kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira yake. Hali hiyo ndio huonyesha mtazamo wake kuhusu masuala mbalimbali anayoyasimulia. Mhakiki anaweza kukadiria ni masuala gani anaunga mkono ama anayakashifu katika jamii ya uandishi. Msuko kioo basi hutilia mkazo matukio muhimu katika riwaya. Kwa mfano,

ingawa tumeelezwa matukio ya msiba wa mhusika kimbele, katika mazungumzo kati ya Mwanatenga na mumewe Amanulla, matukio haya yanasisitizwa zaidi hatimaye kupitia msuko wa kioo.

Msuko wa kioo pia umetumiwa pia katika *Kisima cha Giningi* katika Sura ya Kwanza ambapo Sajin Paolo anamweleza Spekta Seif kumhusu Mwana wa Giningi. Sajin Paolo anaelezwa kwamba, alikutana na Mwana wa Giningi na akamhimiza aende haraka nyumbani kwake. Alidhamiria kufanya uchunguzi kuhusu uhalifu ambao ulikuwa umetokea. Katika ukurasa wa 15 tunaelezwa kuwa, Spekta Seif alikuwa akimweleza Bwana Musa kumhusu Mwana wa Giningi na jinsi alivyopiga ripoti jana kuwa alikuwa kaibiwa. Msuko huu si wa moja kwa moja. Kulingana na nadharia ya umtindo, mtindo humbainisha mtunzi wa kazi za kifasihi pamoja na waandishi wengine wa kazi ya bunilizi. Hii ni kwa sababu tayari tumeelezwa mbeleni kuwa Mwana wa Giningi alikuwa ameibiwa na vilevile Bwana Musa alikuwa ameambiwa kile kilikuwa kimetokea. Aina ya msuko wa kioo, humwezesha msomaji wa fasihi kupata habari za nyumba ambazo humwezesha kuelewa tukio la sasa kwa njia ya uwazi zaidi.

Wakati Mwana wa Giningi anamngoja Spekta Seif ambaye alikuwa amemwahidi kuwa atakwenda kwake asubuhi ile na wakati ule, mawazo mengi yanampitikia Mwana wa Giningi. Fikra hizi za Mwana wa Giningi alipokuwa amesimama nje ya nyumba yake na mtungi wake mkononi tayari kwenda kisimani, zimeelezwa kupitia msuko changamano. Kwanza, alimkumbuka siku hiyo marehemu babake Makame wa Makame alipomkabidhi kisanduku na akamwambia akiba hiyo alitakiwa kuiweka vyema kwa manufaa yake. Pia, Mwana wa Giningi alikumbuka namna siku hiyo ambayo baba yake alipomwamsha kutoka katika usingizi na kumjulisha kuhusu ‘kisanduku hicho.’ Mwana wa Giningi alikiona kikiwa na dhahabu nyingi. Alikihifadhi hadi siku iliyofuata:

> …alikumbuka alipokuwa mkubwa na kuvunja ungo; alikumbuka baba yake alipowacha hizo nyendo zake zisizokwisha; alikumbuka arusi yake na Vuai ambaye sasa wapo mbalimbali. Kwa muda mdogo tu baada ya arusi yake, baba yake alishikwa na ugonjwa wa kufa. Siku moja alipokuwa yupo kitandani kwake anampepea – kwani maradhi yake yalikuwa ya joto- alimsikia sauti yake pole pole ikimwita, naye akatega sikio na kumsikiliza… (*Kisima cha Giningi*: 21)

Mwandishi anatumia mbinu ya kisengerenyuma kumchorea msomaji maisha ya awali ya Mwana wa Giningi. Pia mwandishi anampa msomaji taswira ya maisha ya baba yake mzazi. Kwa njia hiyo, mwandishi anamjengea msomaji matukio yaliyopelekea kifo cha baba yake mzazi wa Mwana wa Giningi. Usimulizi kioo unamsaidia msomaji kugundua, maisha ya utotoni ya mhusika mkuu. Matukio hayo yameendeleza kupitia msuko wa kioo na kusababisha kukamilishana kwa matukio ya kitambo na yale ya kisasa. Kupitia mbinu ya kisengerenyuma, msomaji wa kazi teule anagundua ni nani alimfanyia Mwana wa Giningi uhalifu na kwa nini. Mwana wa Giningi anakumbuka onyo ambalo alipewa na baba yake mzazi kumhusu ami yake, Ali Makame. Alitahadharishwa kumwogopa, kukimbia mahali alipokuwa na kujitenga naye kama shetani ama 'jini' kwa sababu alikuwa ni mwovu (ni sumu baridi). Japo matukio yamesimuliwa kutoka mwanzo kwa kutumia kanuni na taratibu za muundo wa msuko sahili, matukio mengi yaliyosimuliwa si ya moja kwa moja japo yanakamilishana. Kupitia msuko kioo kunakuwa na kasi katika usimulizi kuhusu riwaya teule. Mwandishi anautumia kujenga hamu ndani ya msomaji. Kulingana na nadharia ya umtindo, matumizi ya lugha na fani huhusiana na jinsi mwandishi wa fasihi anavyoibua na kuzungumzia maudhui na dhamira mbalimbali katika kazi yake.

Nadharia ya naratolojia pia hutilia maanani suala la wakati wa kusimulia. Kila tukio hutendeka katika wakati maalum. Nadharia hii basi hujishughulisha na kuangalia 'wakati –hadithi' na 'wakati-matini.' Dhana ya wakati-hadithi huhusu muda ambao hadithi inachukua kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kisa. Inaweza kuwa siku, miezi ama miaka. Wakati-matini hurejelea muda ambao kazi fulani inachulkua kusomwa na msomaji fulani. Hili ni suala la mtu binafsi kwani kila mtu ana uwezo tofauti wa kusoma ama kasi. Hata hivyo, vipengele hivi viwili huhusiana wakati mwingine katika masimulizi. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, ukurasa wa 54, Spekta Seif anamweleza Bwana Msa kilichojiri wakati akimhoji Vuai.  Vuai hakuhusika katika kifo cha mke wake kule kisimani. Mazungumzo yanachukua mkondo wa kishirikina juu ya uchawi. Kulingana na Bwana Msa, hakuna uchawi bali ni imani ya watu tu:

> …nilipokuwa mdogo, nakumbuka nilikuwa siachiwi kutoka nje ila nivae kigwe cha hirizi zinapata tano shingoni kwangu. Na nikifanya ishara ya baridi baridi kidogo tu, mama yangu huniremba masizi uso mzima, nikababakishwa macho tu. Hayo ndiyo malezi tuliyokulia nayo, na bado hayo yapo mpaka sasa kwa baadhi ya wazee na watoto wao. Huo ndio msingi wa

> malezi yetu, mpaka tukapata hiyo elimu ya Kizungu isiyosadiki mambo hayo. (uk. 56)

Kupitia dondoo hili, Bwana Msa anatumia maelezo yake kubainisha kwamba, utamaduni wa mtu hauwezi kufifishwa na elimu na utamaduni wa kigeni. Jamii ya Giningi bado ina itikadi za kitamaduni na bado inaamini katika masuala ya ulogi na hivyo mwandishi anamtumia mhusika huyu kubainisha maudhui ya kishirikina katika riwaya hii. Anafanya hivyo bila kuyasimulia mwenyewe moja kwa moja. Kisa cha Bw Msa kuhusu mama yake kinalenga kudumisha na kuthibitisha imani yake Bw Msa kuhusu dhamira inayohusu itikadi za kijamii kuhusu suala la uchawi. Mwandishi huyu anatumia wahusika kusimulia matukio na kubainisha mawazo yake kwa msomaji. Mama yake Bw Msa alikuwa ameweka vifuu vya nazi. Bw Msa alipotumia kifuu na baada ya haja kukirudisha pamoja na vingine na hatimaye kikapatikana na mama yeke, ilifasiriwa kuwa ni uchawi. Mamake alipoona kifuu hicho, alienda kwa mganga kutafuta ugunduzi. Hali hiyo ilileta ugomvi na tofauti baina ya mama na kaka yake. Mwandishi anamtumia Bw Msa kusisitiza kuwepo kwa ushirikina na itikadi za kitamaduni katika jamii hii. Maneno hayo ya Bwana Msa yalimthibitishia Spekta Seif kuwa, imani kuhusu itikadi hasi zinaweza kuitenganisha jamii. Kulingana na nadharia ya umtindo, mbinu za lugha na fani kwa huathiri kwa kiwango kikubwa jinsi ujumbe unaowasilishwa hufasiriwa na msomaji wa kazi za kifasihi. Tunapata kwamba, ijapo simulizi hizi za Bwana Msa kwa Spekta Seif zimeelezwa ili kuendeleza msuko mkuu wa hadithi nzima, mtiririko wake umejikita katika visa vya zamani na kuyafanya masimulizi haya katika Sura ya Sita kuwa katika msuko changamano.

Msuko changamano unajitokeza vilevile katika Sura ya Kumi na Moja ya riwaya ya *Kisima cha Giningi.* Tukio husika ni kati ya Spekta Seif na Bwana Msa Bw Msa mjini Kikwajuni. Spekta Seif alikuwa amerejea kutoka hospitalini ambako alikuwa amelazwa kwa muda. Mwandishi anatumia kifaa cha redio kutangaza kuadhibiwa kwa Ali Makame na genge lake kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Redio inakuwa nyenzo ambayo mwandishi huyu anaitumia kusimulia hatima ya wahalifu hawa kuhusu tabia yao hasi. Ingawa asasi za kijamii zinashindwa kuwaadhibu, dunia inawaadhibu. Mbinu hiyo pia inatumiwa na mwandishi kumpa mhusika bw Msa nafasi ya kuelezea udhaifu wa asasi ya polisi katika kupigana dhidi ya uhalifu katika

jamii ya Giningi. Pia inampa msomaji ushawishi kuhusu kuwa na upelelezi huru katika jamii ili kusaidiana na asasi za polisi ili kumaliza uhalifu.

Ijapo tumegusiwa kuhusu kisa kilichotokea pale katika *Kisima cha Giningi*, Bw Msa anasimulia matukio hayo upya kuanza pale ambapo Ali Makame alipokwenda nyumbani kwa Mwana wa Giningi. Msa anadhihirisha ya kuwa, Vuai hakuwepo nyumbani kwa Mwana wa Giningi wakati huo:

> …kwa hivyo alijizatiti, akajisogeza kule kunako mdomo wa handaki utokeao kisimani tangu mapema, akakaa kimya kungojea. Lazima alingojea sana, maana Mwana wa Giningi siku ile alikuwa ni wa mwisho kwenda kisimani… tena kwa bahati nzuri kwake alimsikia na akamwona akigombana na mumewe humo kisimani...Ali Makame aliona dunia imempa uso kwani atapata kufanya ukatili wake na tuhuma atatupiwa huyo mumewe ... (uk. 98)

Inabainika ya kwamba, Ali Makame ndiye aliyemuua Mwana wa Giningi pale katika kisima cha Giningi. Matukio yaliyotangulia na kupelekea Ali Makame kumwangamiza Mwana wa Giningi vilevile yameelezwa. Ali Makame aliuona ugomvi wa Mwana wa Giningi na mumewe Vuai kama kijisababu cha yeye kutimiza njama yake ya kumuua bila kutambuliwa. Mwana wa Giningi alipomaliza kuteka maji na kutaka kutoka ndani ya kisima, tayari Ali Makame alikuwa ametoka mafichoni na alikuwa tayari kuua:

> Kutazama-tazama aliona tambara limetupika–sijui lilikuwa likitumika kwa kata- alilichukua na kumsogelea nyatunyatu yule bibi aliyekuwa anainuka na mtungi wake. Kusimama tu, na Ali Makame kafika. Kwa mkono wa shoto alimziba kinywa kwa lile tambara, na wakati huo huo alipitisha kisu chake kwa mkono wa kulia kwa mbele na kukishindilia kifuani. Yaani, akawa kama kamkumbatia mgongoni kwake...Mtungi ulimwanguka wakati ule ule wa kuziba kinywa. Ali Makame alimzuia hivyo hivyo kitambo kidogo, kisha akamwacha kuanguka polepole. Lakini wazimu wake wa kutombakisha yule bibi na kitu, bado alikuwa nao. Alimchonga mikono yote miwili akapata bangili na pete, kiisha akamkata pua akachukua kipini. Kutaka kuondoka, akasikia mlio wa gari inasimama; akalitupa lile tambara, na katika kupenya katika lile tundu, kipini kilimdondoka. (*Kisima cha Giningi*: 99-100)

Ali Makame ndiye alikuwa na nia ya kumuua Mwana wa Giningi. Msuko wa kioo unaleta picha kamili ya maelezo yanayoelezwa. Kulingana na nadharia ya umtindo, msuko kioo hapa umebainishwa kwa kutumia mbinu ya kisengerenyuma kwa

kurejelea jinsi ambavyo visa vingi vilivyoshughulikiwa hapo awali, vinarejelewa na kufafanuliwa zaidi. Tunajulishwa kuhusu matukio mengi yaliyotokea hapo mbeleni na hata tunakutana na baadhi ya wahusika kupitia kisengere nyuma kwa mfano, Babake Mwana wa Giningi. Mhusika huyu amechangia kuijenga ploti ya riwaya ya *Kisima cha Giningi* na kuendeleza msuko na mtiririko wa matukio yake. Japo matukio yake yamerejelewa tu kwa kufafanuliwa, kuna muumano na muwala kati ya matukio ya wahusika hawa wawili; Babake Mwana wa Giningi na Mwana wa Giningi. Matukio mengi yanayowahusu ndiyo ambayo yanajenga msuko huo kioo. Kupitia tukio hili, msomaji anabainishiwa kugunduliwa kwa maficho ya wahalifu walioongozwa na Ali Makame chini ya kisima.

### 2.2.2 Msuko Mwanzo-Kipeo katika Riwaya Teule

Katika msuko mwanzo-kipeo, mwandishi hutumia taratibu za msuko wa moja kwa moja hadi usimulizi wake ufikie kileleni (Muhando na Balisidya 1976). Usimulizi unapofikia kileleni, unakatizwa ghafla na kumwacha msomaji katika hali ya taharuki. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, usimulizi unafikia kileleni na kukatizwa ghafla. Japo Bwana Msa anamweleza Spekta Seif kumhusu Ali Makame na Mshenga Hamadi wa Kidoti, hatuelezewi kilichojiri hapo baadaye. Kupitia matangazo ya redio, yaliyokuwa yakisikilizwa na Bwana Msa na Spekta Seif, tunafahamishwa kuwa Mshenga Hamadi wa Kidoti alifika kwao salama lakini kwa sababu hadithi inafika upeoni, hatuambiwi hatua walizochukua Bwana Msa na Spekta Seif. Huu ni msuko mwanzo-kipeo. Taharuki inayoibuka inaleta msisimko ndani ya msomaji wa kazi husika.

## 2.2 Hitimisho

Kupitia lengo la kwanza, tuligundua ya kuwa, M. S. Abdulla katika riwaya zake za: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007) anatumia misuko sahili, kioo na mwanzo-kipeo. Kupitia kwa misuko hii, mwandishi ameweza kudhihirisha maudhui mbalimbali waziwazi. Vilevile, mitindo hiyo imebainisha matumizi ya mbinu za lugha ya kisengerenyuma na taharuki kama sanaa muhimu katika uandishi wake. Isitoshe, misuko husika inachangia katika usawiri wa wahusika kimatendo na kiwakati katika riwaya husika. Dhima za wahusika na umuhimu wao unabainika vyema kupitia matumizi ya misuko hii. Pia imebainika ya kuwa, misuko hiyo

inamwezesha mwandishi M. S. Abdulla kuwasilisha dhamira za riwaya hizi kikamilifu bila kumchosa msomaji kwa kutumia msuko wa aina moja.

# SURA YA TATU

# USIMULIZI KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007)

## 3.0 Utangulizi

Katika Sura ya Pili, tulishughulikia dhana ya msuko na aina ya misuko katika riwaya teule za M.S. Abdulla pamoja na athari ya aina hizi za misuko kwa mtindo, maudhui na fani. Katika Sura ya Tatu, tulishughulikia lengo la pili la utafiti wetu. Lengo la pili lililenga kudhihirisha aina za usimulizi ambazo mwandishi M. S. Abdulla anatumia katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.*

## 3.1 Usimulizi kwa Ujumla

Usimulizi ni mkakati muhimu ambao mwandishi wa kazi ya kifasihi hutumia wakati wa kuendeleza kisa ama hadithi (Matundura 2008:3). Kulingana na Matundura, kila kisa ama hadithi huwa na msimulizi ambaye hupewa jukumu la kusimulia matukio. Usimulizi unaweza kutekelezwa kwa njia tofauti mathalani nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu. Msimulizi humpitisha msomaji katika matukio, mandhari, maeneo, kipindi cha wakati pamoja na mtagusano baina ya wahusika na mazingira yao. Kwa hivyo, msimulizi kupitia usimuliaji wake huwa anajenga njia ambazo msomaji au mtazamaji hufasiri matukio yanavyotendeka na yanavyosimuliwa. Kutokana na aina ya usimulizi, msomaji hujihisi kama yuko karibu na yote ambayo yanafanyika katika mazingira ya kazi.

Kuna njia nyingi ambazo mtunzi anaweza kutumia katika kuwasilisha kisa chake. Msimulizi anaweza kuwa ameshuhudia au kushiriki matukio anayoyasimulia (Mazrui na Syambo 1992:75). Msimulizi anaweza kujitokeza bayana na kujitambulisha au akose kujitokeza bayana. Kwa njia hiyo, msomaji wa kazi ya kifasihi huweza kuongozwa kwa matukio muhimu ya kazi. Pia, huwa anaelekezwa kwenye msimamo, maoni, mwelekeo pamoja na suluhu ambayo mwandishi ataitoa kama ataridhia kufanya hivyo. Mazrui na Syambo katika kazi yao pia walieleza kuwa mwandishi anaweza kuamua kutoeleza mambo ambayo hayakudhihirika katika maneno au vitendo vya wahusika. Riwaya zinazotumia usimulizi wa kutoeleza mambo ambayo hayakudhihirika katika maneno au vitendo vya wahusika huwa na mazungumzo mengi. Kupitia mbinu hiyo, fikra na mawazo ya wahusika hayadhihiriki moja kwa

moja. Msomaji huachiwa jukumu la kung'amua bila kuelezwa sababu za vitendo na maneno ya wahusika kwa njia ya kuangalia muktadha.

Namna ambavyo msimulizi hutagusana na kisa ama kazi ya mwandishi husika ndio humwezesha msomaji huyo kutambua aina ya usimulizi wa mwandishi husika (Attenbernd na Lewis 1963). Kulingana nao, ni kupitia hali hiyo ambapo mhakiki wa kazi ya kifasihi ataweza kujua ni nani ndiye anasimulia kisa hicho na kwa njia gani. Msomaji wa kifasihi basi anatakiwa kujiuliza maswali kama: msimulizi ni nani? Ni vizuri kuelewa ni nani anayesimulia kazi hiyo na ana mtazamo gani. Vilevile msomaji anapaswa kuuliza kuhusu uhusiano wa msimulizi na matukio ambayo yanasimuliwa. Isitoshe, anatakiwa kujiuliza iwapo yanamshirikisha msimulizi kwa njia gani? Ni juu ya mhakiki wa kifasihi kutambua iwapo matukio yanayosimuliwa yanaaminika kwa msimulizi na kukubalika ama la. Masuala hayo yaliongoza uchanganuzi wa data kuhusu usimulizi katika riwaya teule za M.S. Abdulla: *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.*

Kwa mujibu wa Wamitila, usimulizi unahusu kueleza matukio katika kisa ama hadithi katika matini za kifasihi (Wamitila 2003). Usimulizi huwezesha mtunzi kuwasilisha mafunzo ya kimaadili kwa hadhira lengwa kupitia kazi yake. Wamitila anapendekeza msomaji wa fasihi kujiuliza ni kwa njia gani kisa husika kimesimuliwa? Wamitila anataja aina zifuatazo za usimulizi: usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili, usimulizi wa nafsi ya tatu, usimulizi maizi, usimulizi penyezi, usimulizi sawia, usimulizi tangulizi, usimulizi wa ki-utendi, usimulizi wa kirejeshi, usimulizi wa kiutomaji, usimulizi anuwai na usimulizi ngazi.

Mlacha anaeleza kuwa, usimulizi ni uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi yenyewe inayosimuliwa (Mlacha 1991). Yeye anasisitiza ya kwamba, njia bora ya kuelewa usimulizi ni kutambua ni nani huyo ambaye anatuwezesha kuipokea hadithi yenyewe katika matini husika. Mawazo yake huenda ndio inamfanya Kanar kusema ya kwamba, usimulizi ni mtindo ambao unahusu mpangilio ambao unatumiwa na waandishi wa kazi za kubuni kueleza matukio mbalimbali katika matini za kifasihi (Kanar 2001). Kulingana naye, kuna kanuni mahsusi ambazo ni sharti msimulizi azingatie. Mojawapo wa kaida hizo ni wakati wa masimulizi. Hadhira ama wasomaji wa kifasihi huwa wanatarajia kuona kaida maalum za mwandishi na namna zinavyochangia katika kufaulisha kazi yake.

Msimulizi basi hatarajiwi kupuuza kaida za kusimulia na kutoka nje ya matarajio ya hadhira inayolengwa. Kulingana na baadhi ya wahakiki, kaida za usimulizi bora zinahusu masuala kama: wahusika ni kina nani? Wanajihusisha na matukio gani? Ni wakati gani wanafanya hivyo? Ni lini hiyo? Ni kwa nini wanafanya wanayoyafanya na kwa njia hiyo? Msukumo wao ni gani? Kwa mujibu wa Baldick, usimulizi ni mchakato ambao unahusiana na usimuliaji wa matukio kwa njia ya kimpangilio na kimfuatano (Baldick 1990). Mawazo ya Baldick na Kanar yadhihirisha kuwa, jinsi masimulizi yanavyotekelezwa na jinsi wahusika wanavyosemezana katika matukio tofauti huchangia kufaulisha kazi ya mtunzi anayechunguzwa.

M.S. Abdulla alisuka riwaya zake kwa kutumia masimulizi mseto. Yeye alichanganya usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi maizi. Usimulizi wa aina hizi umetumika katika riwaya teule za M.S. Abdulla: *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa* mtawaliwa. Aina hizi tatu za usimulizi ndizo tulizishughulikia katika utafiti wetu katika riwaya teule za M.S. Abdulla na pia tulikita maelezo yetu kwa maoni ya watalaamu mbali mbali akiwemo Plato na wengine wa kipindi cha hivi karibuni.

### 3.2 Daigesia

Kama anavyoshadidia Wamitila, nadharia ya Naratolojia iliwekewa msingi na Plato katika kazi yake ya, *Republic* (Wamitila 2002:139). Plato alizungumzia usimulizi katika hali ya *mimesia* na *Daigesia.* Katika daigesia, msimulizi anabainika kwani anajitokeza waziwazi. Huu ni usimulizi wa nafsi ya kwanza. Ni mbinu inayowasilisha hadithi kama ambayo imesimuliwa na mmoja wa wahusika wake. Kunakuwa na matumizi ya ‘ni’; kiwakilishi cha nafsi ya kwanza. Mhusika anaweza kuwa nguli ambaye anasimulia hadithi yake mwenyewe, ama akawa mhusika mdogo tu akieleza yaliyomkumba nguli. Mhusika huyu anaweza kuwa mshiriki wa matukio au matendo ya hadithi au akose kuwa mshiriki. Aina hii ya usimulizi hujenga uhusiano wa karibu kati ya hadithi na msomaji (Mazrui na Syambo 1992). Usimulizi huu humfanya mwandishi na msimulizi kuwa kitu kimoja machoni mwa msomaji wa kazi inayochunguzwa. Msimulizi na mwandishi huwa wamekaribiana sana kinafsi. Mhusika msimulizi huwasiliana na msomaji moja kwa moja bila kupitia maelezo ya mhusika mwingine.

Yanayosimuliwa huwa sio mawazo binafsi ya mwandishi wa matini za kifasihi zinazochunguzwa. Kauli yetu inashadidia mawazo ya Carpenter na Neumeyer (1974: 184) Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, mwandishi ametumia mbinu ya barua kwa ufundi mkubwa. Ni katika mbinu hii ambapo usimulizi wa nafsi ya kwanza unajitojkeza kidhahiri:

> Mimi sasa nimepata uhamisho kuja huku Giningi, pahala panaposifika kwa uchawi- na kweli; maana, hata mazungumzo ya watu wa huku ni uchawi na kulogana…. Tafadhali ninakutarajia siku ya Jumatatu, ufike hapa asubuhi, na hata chai yako njoo unywe huku. (uk. 8)

Kulingana na dondoo, Seif na Bwana Msa ni marafiki wa muda mrefu na wanajuana vyema. Waliwahi kukutana awali katika *Mzimu wa Watu wa Kale*. Seif mbali na kumkumbusha bwana Musa kuhusu ufanisi wa upelelezi wake, anataka amsaidie kutatua kesi nyingine huko Giningi. Mwisho Seif anamwambia Bwana Msa kuwa amehamia Giningi na anamwalika kwake Jumatatu. Usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumika katika dondoo hili kwa kuwa kuna matumizi ya viambishi vya nafsi ya kwanza; ‘mimi’ na ‘ni’. Kupitia dondoo hili, tunalazimika kufuatilia mtiririko wa riwaya nzima kwa karibu. Mwandishi anajenga taswira ya ushirikiano baina ya Msa na Seif na namna watu binafsi na asasi za umma hushirikiana kufanya kazi. Sifa za wahusika hawa wawili na uhusiano wao pia unabainika. Ni kupitia kwa mhusika msimulizi ambapo wasomaji wanayaelewa maudhui ya kazi kupitia kwa mtazamo wa wahusika. Hadithi inayotumia usimulizi wa nafsi ya kwanza huwa hai zaidi kwani huifanya hadithi ifanane na maisha ya kila siku. Vile vile katika usimulizi huu, mwandishi anafichua mambo ambayo msimulizi wake hakuwa anayatambua pale awali mpaka pale ambapo yatahitajika katika mtiririko wa vitushi.

Katika mbinu hii ya usimulizi, mwandishi huipoteza nafsi yake kwa mhusika simulizi ambaye husimulia hadithi yote ama sehemu yake kwa jicho la kwanza. Kwa mfano Bw Msa katika riwaya ya *Kisima cha Giningi.* Mbinu hii hata hivyo sio rahisi kuitumia kwa sababu humtaka mwandishi kuwa makini sana wakati anatumia viwakilishi vya nafsi: ‘ni’ na ‘mimi’ ili asizitumie kupita kiasi. Matumizi mengi ya nafsi hizo yanaweza kuwachosha wasomaji (Mohamed 1995: 52). Katika riwaya teule za M.S. Abdulla, mwandishi ametumia mbinu hii kwa uchache sana.

Usimulizi huu humbana sana mwandishi kwani kuna mambo mengi sana ambayo hawezi akayaeleza bayana. Haya yanadhihirika bayana katika riwaya teule. Kwa

mfano, katika *Kosa la Bwana Msa*, Jamila anayaeleza matukio alipokuwa Dubai kupitia barua alizomwandikia rafikiye Mwanatenga kwa kudokeza tu wala si kwa ufafanuzi wa kiundani. Hii ni kwa sababu matukio yanatokea kiwakati; yaani tukio moja baada ya lingine na itakuwa vigumu matukio yote kuelezwa kwani tunalazimika kutazama mambo kupitia kwa mtu mmoja. Mhusika msimulizi ndiye tunayemtegemea kutueleza mambo ambayo hatuyashuhudii wenyewe. Katika riwaya teule tunawategemea sana wahusika kama Bwana Msa, Jamila na Mwanatenga kueleza matukio mbalimbali kwa niaba ya mwandishi. Jambo hili linaathiri jinsi matukio yanavyoelezwa sababu hayajabainika waziwazi na wala si matukio yote yameelezwa. Mwandishi anaweza kuamua kutumia mazungumzo baina ya wahusika, barua au mbinu ya kisengere nyuma ili kutupanulia mtazamo na shabaha ya kazi yake.

Waandishi hujitenga na utata huu kwa kuwataja wahusika wasimulizi kwa majina yao. Licha ya waandishi kujitenga mbali na mhusika msimulizi, hii inabaki kuwa kazi ngumu kwao kwani waandishi ni watunzi wa hadithi na hawawezi kutenganishwa na mhusika msimulizi kwa urahisi. Kwa hivyo, ni makosa kuyaoanisha mawazo ya msimulizi wa nafsi ya kwanza na yale ya mwandishi kwani msimulizi kama huyo ni mhusika kama wale wengine hadithini na wala si lazima awe msemaji wa mwandishi. Hata hivyo, mbinu hii ina ubora wake.

Dhana hii ndiyo inayotuelekeza zaidi kutazama hadithi yoyote inayosimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza kama inayosimuliwa na mwandishi mwenyewe. Swala la mhusika anayesimulia kupewa jina tofauti na mwandishi hakika haliwi dhihirisho tosha kwa wasomaji na haliwafungi macho katu kwa kuwa mwandishi ana uhuru wake wa kuwachagua wahusika jinsi apendavyo. Kwa mfano, mwandishi M.S. Abdulla ametumia majazi kuwapa wahusika wake majina ili kuendeleza matukio ambayo yeye mwenyewe ameyajenga. Majina haya huwa ya kimajazi ama lakabu kulingana na sifa na umuhimu wao. Kwa mfano, katika *Kisima cha Giningi*, mwandishi amewatumia wahusika kama Mwana wa Giningi na Spekta Seif. Jina la Mwana wa Giningi limetumika kimajazi kudhihirisha usuli wake. Yeye kitovu chake ni Giningi. Jina la Spekta Seif linadhihirisha cheo chake na asasi anayoiwakilisha katika kazi husika.

Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, kuna msururu wa barua ambazo Jamila alimwandikia Mwanatenga, Jamila akiwa Dubai kwa mfano: Ninajua una hamu kubwa ya kupata barua yangu, kama mimi nilivyo nayo ghamu si ndogo ya kutaka kukuandikia. (uk. 106)

Jamila, katika barua hii, anatuingiza katika mawazo ya Mwanatenga na kutujuza kuhusu hisia zake. Tunajua kuwa Mwanatenga ana hamu ya kukutana na rafiki yake, Jamila.Walikuwa wametenganishwa kutokana na safari ya Dubai. Kusimulia ni kueleza matukio kwa njia ya utendekaji wake yawe ya kubuni ama halisia. Kulingana na Gennette (1980), nadharia ya usimulizi huelezea hali tatu ya usimulizi: kuelezea kauli ya kimaandishi ama kisimulizi iliyokusudiwa kuelezea tukio fulani (Wamitila 2002:139). Hii ina maana kuwa, mhakiki huangalia dhamira ya msimuliaji katika matukio yanayoelezewa. Genette aidha anasema kuwa, naratolojia huchunguza mfuatano wa matukio katika kazi za kibunilizi ili kutambua kiini cha usimulizi husika na kubainisha maana kama inavyojibainisha katika kazi za mwandishi huyu.

Katika sehemu nyingine, usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumiwa vilevile:

> Nimemfuata, ndugu yangu, huko kiwanda chenyewe kilikuwa cha magari. Akaingia ndani, kisha karudi kuniita. Tulipofika katika behewa hilo kubwa lililojaa magari mapya mapya, yote yamevaa karatasi za upya, hayajavuliwa. Nikamsikia yeye ubavuni kwangu akisema, "Hili lako." (uk. 106).

Kulingana na dondoo hili, Jamila anatuingiza katika mandhari ya behewa walipoenda na Aziz mume wake na kutujuza kilichokuwa kikiendeleza. Kulingana na nadharia ya umtindo, matini inavyoaandikwa hutegemezwa miktadha maalumu ambayo pia huibua upekee wa matumizi ya lugha Crystal na Davy (1969:10) Kwa hivyo, uelewa wa matini fulani humlazimisha msomaji au mhakiki kuzingatia muktadha wa matumizi ili kuweza kubainisha maana iliyokusudiwa na mwandishi. Mbinu ya jazanda inajibainisha katika fikra ya msomaji kupitia usimulizi huu kwani tunachorewa taswira katika behewa; jinsi magari yalikuwa mapya. Pia, tunapata sura kamili ya upya wenyewe anaposema kuwa hayajavuliwa upya wake kutokana na kuwa bado yana makaratasi yaliyofunikiwa. Wahusika pia wanajengeka kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Katika *Kosa la Bwana Msa* ukurasa wa 108, kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi ana uwezo wa hata kutufahamisha kuhusu wahusika wengine. Ndio mwanzo tunapatana na mhusika Akaz. Ana uwezo wa kueleza kuhusu mandhari, wakati na mahali wanamopatikana wahusika wengine ila

usimulizi huu unabana sana na hauwezi kueleza matukio yote yanayofanywa na wahusika wenzake. Kwa mfano, wakati Jamila anamweleza Mwanatenga kuhusu mhusika mwenzake Aziz, Akaz haelezwi kabisa. Matukio yake hayaelezwi wala hatuambiwi mandhari na mahali alipokuwa. Katika barua ya tatu anayoandikiwa Mwanatenga, Jamila anasema:

> Sijui nikwambie nini, Mfano wake ni kama nimejaliwa kuona nyota ya jaha, maana kila siku kukicha Mungu ananifungulia neema zake tu. Labda vile nilivyokaa nikimshukuru tu yeye Bwana, ndio akanizidisha namna hii. Kwani hakusema mwenyewe katika Kurani yake tukufu: Mkishukuru, ina, nitakuzidisheni
>
> ...juzi Aziz alituchukua mimi na Akaz, tukaenda kuonana na wakili, mwanasheria. Huko nilijulishwa naye bwana huyo, mtu mmoja makamu, mpole, hana makuu ya utukufu wa kazi yake, anaitwa Khaazin. (uk.110- 111)

Hapa tunafahamishwa habari zaidi kuhusu wahusika Akaz na Khaazin. Akaz ni mwanawe Jamila ambaye anataka awe mrithi wake atakapokuwa mtu mzima. Khaazin ni wakili wa Aziz ambaye ndiye angehalalisha urithi huo. Kama tulivyoeleza awali, pia ni dhahiri katika dondoo hili jinsi msimulizi anavyojiunga na wahusika wengine kutufahamisha vitendo vilivyokuwa vikiendelea. Kwa mfano, msimulizi ameungana na Jamila, Akaz na Aziz kuandamana nao kwenda kwa Khaazin. Kila tukio analolieleza analishuhudia.

Gennette anasema ya kwamba, nadharia ya naratolojia hujihusisha na kuelezea tendo lenyewe la kusimulia katika kazi ya kifasihi na kama anavyoshadidia (Wamitila2002: 139). Katika aina hii ya usimulizi, mwandishi huwatumia wahusika kusimulia kuhusu wahusika wenzao na hivyo kumsaaidia msomaji kujua hulka zao ambazo hazijaelezwa na mwandishi katika matini (Mlacha 1991). Wahusika huwa na uwezo wa kutaja sifa tofauti za wenzao kupitia mazungumzo na mtagusano wao. Mwandishi M.S. Abdulla amemtumia Jamila kutufahamisha hulka za wahusika kama vile Khaazin na mitazamo yao kuhusu masuala mbalimbali. Kwa mfano, kupitia barua hii ya tatu, tunajuzwa kuwa Khaazin alikuwa mpole na alikuwa akiipenda kazi yake sana. Kulingana na nadharia ya umtindo, lengo la mwandishi kuhusiana na maswala ambayo anataka kuyaibua ndiyo humuamulia mtindo atakaoutumia (Senkoro 1988:6). Kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza, tunagundua kuwa, katika aina hii ya usimulizi, msimulizi hupewa kipaumbele kuendeleza mtiririko wake ikilinganishwa na wahusika wengine ambao wanaelezwa tu kupitia mhusika msimulizi.

### 3.3 Usimulizi wa Mimesia

Huu ni usimulizi wa nafsi ya tatu humpa mhusika mmoja nafasi ya kusimulia hadithi badala ya msimulizi mwakote kuisimulia yote (S. A. Mohamed 1995). Katika *mimesia*, msimulizi hajitokezi waziwazi. Mhusika mmoja ndiye hupewa wakati kuendeleza masimulizi ya hadithi na kusimamia mawazo ya mwandishi. Hata hivyo, baadhi ya waandishi huzichanganya mbinu za usimulizi katika kazi zao (Wamitila 2003). Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, mwandishi hutumia viambishi vya nafsi ya tatu (Mazrui na Syambo 1992). Usimulizi wa nafsi ya tatu hutambuliwa basi kutokana na matumizi ya nafsi "ali-." Msomaji hupata matukio kwa kumtegemea msimulizi pekee kwani ni yeye msimulizi ndiye anashuhudia matukio yote.

Tofauti na usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu huwa unatoa nafasi kubwa kwa wahusika wengi kushiriki pamoja na kuendeleza mtiririko. Msomaji hana uwezo wa kutaka au kupendelea mambo fulani yafanyike. Uwezo huu ni wa msimulizi peke yake na matukio yanayoelezwa kama atakavyo mwandishi. Ijapo usimulizi wa aina hii huwa una utata kwa msomaji na msikilizaji, usimulizi huu humrahisishia msomaji dhana ya kiwakati na kijiografia katika kazi husika. Pia, haumchoshi msomaji kwa sababu mazingira ya usimulizi huwa yamebanwa sana. Hata hivyo, wasomaji hupata athari tofauti tofauti. Baadhi huwa ni kuona ufupi wa masafa ya kijiografia na kiwakati ya kazi. Baadhi aidha hudhani kuna kubanwa kwa msuko.

Dhamira kuu ya natatolojia ni kuangalia sifa za simulizi na kuzidhihirisha na sifa nyingine katika matini zinazochunguzwa. Nadharia hii huchukulia kuwa, kila usimulizi huwa wa tabia fulani ama kuongozwa na kanuni fulani. Baadhi ya wahakiki wanasema kwamba, nadharia hii basi huangalia umuundo wa kazi husika. Swali kuu kwa wananaratolojia huwa ni, kazi husika ina mwelekeo gani? M.S. Abdulla ametumia nafsi ya tatu kwa ufundi mkubwa ili kudhihirisha malengo yake waziwazi. Ni kupitia katika usimulizi wake ambapo mtiririko unajengwa kutoka tukio moja hadi lingine. M.S. Abdulla katika riwaya teule ameweza kujenga uhusiano kati yake na hadhira husika hivyo basi matukio anayoyaeleza yameeleweka vyema. Ufundi huu ndio unamwezesha mwandishi wa riwaya teule M.S. Abdulla kuumba, kuisuka na kuiwasilisha kazi yake kwa namna ya pekee. Riwaya teule za M. S. Abdulla: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007) zinasimuliwa na kuegemea sana usimulizi wa nafsi ya tatu. Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Musa*:

> Jamila alistaajabu kuona katika gari lile anateremka bibi mmoja wa Kiarabu, mweupe pe, mzuri kwa namna yake, na ana haiba ya kumtia mtu fadhaa ya roho. Bibi yule kwa upande wake naye, aliona kasimama mlangoni pale, mtoto mwanamke mzuri kama malaika, mwenye uzuri uliompiga machoni mwake, ukamtia kiwi cha macho- hata ikampitikia moyoni mwake, "Ikiwa mwanamke mwenyewe ndiye huyu! (uk. 7)

Kulingana na dondoo hili, bibi mmoja wa Kiarabu anawasilisha tisho la kumwonya Jamila. Mwandishi anatueleza pia bibi huyu alikuwa mwenye haiba ya kumtia mtu kiwewe. Taswira iliyoibuliwa ni dhihirisho ya kuwa, bibi anayeelezwa ni wa tabaka la juu hivyo kusaidia kuyajenga maudhui. Matumizi haya ya viwakilishi vya nafsi ya tatu ni dhihirisho kuwa, mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu katika masimulizi yake. Kwa mfano anasema; 'Jamila alistaajabu…'

Usimulizi wa aina hii humwezesha mwandishi wa kifasihi kusimulia matukio yote pamoja na matokeo kwa wakati mmoja. Yaani, mwandishi anaweza kuingia bongoni mwa mhusika na hata katika moyo ama nafsi yake na kueleza mawazo na hisia za wahusika mbalimbali. Mawazo, hisia na vitendo vya wahusika huelezwa na msimulizi aliyejibana pembeni na kutazama kwa jicho la tatu. Mwandishi huwa amejipunguzia mzigo wa kumwelezea msomaji mengi ambayo anayoyafahamu kwa njia ya kumtumia mhusika mmoja peke yake. Yote anayoyajua ni kumhusu huyo mhusika na haonyeshi kuwafahamu wahusika wake wengine. Kwa hivyo, mawazo, mwelekeo na msimamo wa mhusika huyo mmoja ndio utambuliwao na mwandishi kwa undani. Hapa mwandishi huwa amejipunguzia uhuru wake wa kuyaeleza yote anayoyajua kuihusu hadithi yake. Mhusika anayepewa nafasi hiyo anaweza kuwa mhusika mkuu au mhusika mdogo katika hadithi husika. Mhusika aliyepewa uwezo huu katika riwaya teule ni Bwana Msa. Ni yeye ndiye ambaye anafahamu maafa yaliyotokea ndiposa Mwana wa Giningi akauawa na Ali Makame.

Nadharia ya Narotolojia huchunguza masuala matatu katika usimuliaji ambayo ni: usimulizi, hadithi na tatu, usimuliaji. Usimulizi huhusu utambaji wa tukio. Yaani, namna mwandishi anavyoisuka hadithi yake. Hivi ni vitu viwili vinavyoingiliana na bila hivyo, kazi husika itakuwa chapwa. Hadithi kwa upande mwingine, ni matukio yaliyosimuliwa na mwandishi ama mtambaji. Huwa yamesukwa katika mfuatano wa kiwakati.

Usimulizi wa ki-mimesia unampa M.S. Abdulla uhuru wa kueleza matukio yake kikamilifu na kwa njia ya upekee. Usimulizi wa aina hii hutambulishwa na matumizi ya "ali-" jinsi ilivyobainika. Katika dondoo hili, ni kupitia msimulizi wa jicho la tatu ndiye ambaye anasimulia matukio ya wahusika wengine. Matukio katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* yameelezwa kwa uwazi zaidi. Kwa mfano, kuwahusu Jamila na bibi mwenye asili ya Kiarabu aliyekuja kumwonya Jamila. Maelezo haya ndiyo yanaendeleza matukio tofauti hivyo kudhihirisha muwala wa vitushi:

> Eh! Jamila aliona mambo makubwa yamemfikia tangu kaolewa na Bw. Ali, huu sasa ni mwaka wa tatu na miaka yote hiyo anakaa katika nyumba ile ile. Hakupata kufikiwa na jambo kama lile la kujiwa kwake na mtu ajinabi asiyekuwa na haya, mkavu wa macho, mtu safihi kama yule. Miaka yote hii aliyokaa hapa, yeye ameendeshana na watu kwa heshima na adabu- yeye anawaheshimu, na wao wanamwekea adabu yake na staha. Lakini leo kafikiwa! Anakusudia nini bibi huyu hasa! Bibi yule alitaka kujitoma ndani, lakini alipofika kizingitini, alisita akasimama kwa ghafla, macho yake juu ya picha iliyokabili mlango, na iliyomkabili yeye usoni kwake! Baada ya muda kitambo, na kushusha pumzi, aliingia ndani akakaa juu ya kiti kuikabili picha ile. (uk. 8)

Kupitia dondoo hili, tunamwona yule bibi mwenye asili ya Kiarabu akitaka kuingia kwa nguvu ndani ya nyumba ya Jamila na kukabiliana naye. Matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu *ali*- vinazidi kudhihirisha kuwa usimulizi ni wa nafsi ya tatu. Mfano mwandishi anaposema; 'Bibi yule a*li*taka kujitoma ndani…' Usimulizi wa nafsi ya tatu unamwezesha mwandishi kuwa na uhuru wake wa kuteua maneno na haujambana hata kidogo kujieleza. Hali isingekuwa hivyo ikiwa mwandishi asingetumia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Matukio kuhusu wahusika tofauti yameelezwa bila kujali mipaka ya kiwakati na kijiografia. Sifa za wahusika hawa pia zimejidhihirisha. Kupitia dondoo hili, ni dhahiri kuwa, vitendo vya bibi huyu vinabainisha sifa yake ya ufidhuli. Sifa zake ni kinyume kabisa na sifa za Jamila ambaye ni mvumilivu na mwenye staha kwani katika maelezo tunafahamishwa kuwa alikuwa anaendeshana na wandani wake kwa adabu (*Kosa la Bwana Msa* uk. 9). Tunaelezwa ya kwamba, alipokuwa akiondoka kwa Jamila, alimsukuma Jamila kwa mkono wake ghafla kama njia ya kumdhalilisha. Pia anamtolea dereva wake amri ya kuendesha gari kuelekea mjini. Kupitia dondoo hili, sifa za bibi huyu zinabainishwa. Ni mtu mwenye majivuno kwa jinsi ambavyo alimsukuma Jamila alipokuwa akiondoka. Kulingana na nadharia ya umtindo, jinsi ujumbe unavyopitishwa katika

kazi ya fasihi na kuifikia hadhira lengwa kwa njia ya kuathiri hutegemea mbinu za msanii katika matumizi ya lugha na fani kwa ujumla. Usimulizi wa aina hii humsaidia msomaji kuelewa hulka ya wahusika katika kazi ya kifasihi. Isitoshe, huwaainisha wahusika kulingana na nafasi zao katika jamii. Msomaji anaweza kubainisha tabaka la mhusika na kwa nini anatenda matendo kwa namna anavyoyatenda. Pia, tunabainishiwa tabaka la bibi huyu. Anamiliki shangingi, ana dereva wake maalum na pindi anapojitoma garini, neno moja la amri linadhihirishia dereva wake anachopaswa kufanya. Aina hii ya usimulizi humfanya msomaji afuatilie moja kwa moja matukio katika riwaya teule za M.S. Abdulla.

Mojawapo wa mihimili muhimu ya nadharia hii ni kuwa, simulizi na hadithi huwasilishwa kwa njia mbalimbali na zilizotofautiana. Kwa mfano, msanii anaweza kufanya hivyo kwa kutumia ushairi ama riwaya kama huyu mwandishi ambaye tulichunguza kazi zake. Uchunguzi bora wa usimulizi basi ni sharti uonyeshe tofauti hizo. Nadharia hii inasisitiza kwamba, ni sharti mchunguzi kuhakiki kinachosimuliwa, matukio yenyewe pamoja na usimuliaji wenyewe na namna ulivyotekelezwa. Kwa njia hiyo, mhakiki ataonyesha kufanikiwa ama kutofanikiwa kwa msanii. Katika sura ya kwanza ya riwaya ya *Kisima cha Giningi*, mwandishi anadhihirisha usimulizi wa nafsi ya tatu. Tunasoma:

> Bwana Msa alimkuta Spekta Seif katika hali ya kumngoja. Si kwa kuwa yeye kakawia kufika, bali yeye mwenyewe Seif hana desturi ya kulala asubuhi ijapokuwa alikuwa nayo nafasi ya kujipumbaza kwa uvivu huo ambao watu wengi wengine huukaribisha. Bwana Msa vile vile alijihimu, akaingia katika gari ya awali; kwa hivyo, alifika Giningi inapata saa thenashara asubuhi. Hakupata taabu ya kuitafuta nyumba ya Spekta Seif, kwani alipomwambia dereva amteremshe stesheni ya polisi, kufika tu dereva alimwambia ateremke. (uk. 9)

Kupitia dondoo hili, wahusika Bwana Msa na Spekta Seif wanakuzwa. Kwanza, ni wahusika ambao ni marafiki wa dhati. Pia, wana uhusiano mwema. Bwana Msa anapopata mwaliko wa Spekta Seif hasiti kufika kwake. Sifa moja kuhusu usimulizi wa nafsi ya tatu ni kuwa msimulizi husimulia matukio ambayo yeye katu hakushiriki. Anaeleza walivyofanya watu wengine, kwa hivyo viambishi 'a', 'wa', 'yeye' na 'wao' vinatumika kwa wingi. Hivi ni viambishi vya nafsi ya tatu ambavyo vinatambulisha usimulizi huu jinsi inavyobainika. Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, hali hiyo inabainishwa ifuatavyo:

> Waliliona gari lenye rangi ya maziwa likiongoza njia Malindi, na wao wakatia moto gari lao wakaanza kulifuata… Walipofika Mikunguni, gari la mbele lilisimama mbele ya stesheni ya mafuta likawa linajaza mafuta; la nyuma nalo lilisimama likaacha masafa yao yako pale pale….uk 60. Hawakwenda mbali sana. Hawakutimiza hata maili moja zaidi mara walililiona gari mbele yao, kwa ghafla, limebwaga katika mwendo wake mkubwa lililokuwa nalo… (uk. 61)

Kulingana na nadharia ya umtindo, ujumbe humsukuma msanii wa kazi za kifasihi kuteua mtindo fulani. Kulingana na dondoo, msimulizi amejitenga faraghani huku akisimulia matukio ambayo hahusiki nayo hata kidogo. Matukio haya yanayoelezwa kikamilifu wala haonekani kubanwa anapoeleza anayoyashuhudia. Tofauti na usimulizi wa nafsi ya kwanza, uhusiano kati ya msomaji na kazi husika katika usimulizi wa nafsi ya tatu huwa wa kando kabisa. Anachofanya msomaji ni kujiweka kando na kufuatilia mtiririko wa matukio kwa umakini.

### 3.4 Usimulizi Maizi

Kulingana na Hawthon, aina hii ya usimulizi ndiyo ya kitambo sana ikilinganishwa na nyingine (Hawthorn 1985). Katika mbinu hii mwandishi huieleza hadithi ambayo, mara nyingi, yeye haimhusu. Mwandishi huwa ni mshiriki tu ingawa ndiye muumba wa kisa chenyewe. Mmoja wa wahusika anakuwa na uhuru mwingi sana wa kueleza matukio. Katika *Kisima cha Giningi,* mhusika ambaye amepewa uwezo huu ni Bw Msa. Ana uwezo wa kutamba na kueleza maswala mbalimbali. Mohochi (2000) na Mohammed (1995) wanaeleza aina hii ya usimulizi kama usimulizi ambao msimulizi anaelewa kila kitu kinachotendeka pamoja na mazingira yake na hata wahusika wanaoyatenda matukio. Katika usimulizi wa aina hii, msimulizi huwa na uhuru zaidi. Msimulizi ndiye huamua ni tukio gani la kusimulia na ni tukio lipi dilo la kuacha. Katika Sura ya Kumi na Mbili, Bwana Msa anadhihirisha haya anapomwelezea Spekta Seif kilichotokea. Mhimili mwingine wa nadharia ya naratolojia ni kwamba, sio kila wakati matukio hufuatana kiwakati. Msanii huwa ameyakatiza kwa kutumia mbinu kama kisengerenyuma ama kisengerembele kama njia ya kukumbusha ama kutabiri hatima ya matukio yanayosimuliwa. Katika masimulizi ya kinathari, aghalabu mtunzi hutoa maelezo halisi ya wahusika, mandhari na hata hali zao za kijisaikolojia. Kupitia usimulizi wa aina hiyo, msomaji hupata hali halisi ya matukio na kutambua ni kwa nini mtunzi anasimulia kwa njia husika. Tukio likisimuliwa katika mfuatano wa kiwakati, msuko na pamoja na hadithi yenyewe huwa na

mpangilio sawasawa. Yaani, msomaji anaweza kusema tukio la kwanza ni hili, la pili linafuatia hivi pamoja nay ale mengine kwa mkumbo huo.

Katika usimulizi maizi, mwandishi ana uhuru kiasi kwamba tunamtarajia kuelewa hata mawazo ya wahusika wake. Kwa hivyo, msimulizi huingia katika akili ya mhusika na akatufafanulia mawazo yake. Kama ilivyo katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, msimulizi kupitia mawazo ya Bwana Msa anatueleza mtiririko wa matukio mengi ambayo mwanzoni hatukuyajua. Katika hali hii, mwandishi huwa anachora taswira kamili ya mawazo au msimamo wa mhusika. Mwandishi ndiye anachanganua matendo ya kumpa mhusika msimulizi maizi na hata kumfafanulia waziwazi kinachoyazua matendo hayo. Mhusika kama huyo hupewa uwezo wa tathmini wahusika wenzake na huwa hulka zao zimefafanuliwa barabara. Kupitia aina hii ya usimulizi, huwa mwandishi amefanya uelewekaji wa kazi inayosomwa kuwa rahisi na hata kuyatambua matukio makuu huwa mepesi (Carpenter na Neumeyer 1974).

Kuna wakati mwandishi wa kifasihi huwa anatumia msimamo wake kuhusu wahusika na matukio. Hata hivyo, huwa mara kwa mara anakumbusha wasomaji wake ya kuwa, yeye ndiye aliyeyabuni. Huwafanya wasomaji kutambua ya kuwa, wayasomayo si matukio ya kikweli bali ni ya kubuni tu. Hii ina maana kuwa, mwandishi huwa amejitenganisha na yanayosimuliwa katika kazi. Mara nyingi, matukio yanaposimuliwa bila mwandishi kutoa maelezo, huwa kuna uwezekano wa msomaji kudhani ya kwamba, matukio hayo yanayojifafanua yenyewe. Kwa kufanya hivyo, msomaji anaweza kumsahau mwandishi kama muumbaji wa hiyo sanaa. Kuna pia hatari ya msimulizi kutoa msimamo wake kuwahusu wahusika au matendo yao. Hali kama hiyo humfanya kuonekana kama ambaye anaingilia kati badala ya kuwaachia wasomaji nafasi ya kutafakari na kujiamulia wenyewe ama kufanya uamuzi wao kwa njia huru. Kulingana na Wamitila, usimulizi maizi hutambulishwa kutokana na uelewa kwamba, msimulizi wa aina hii huwa anafahamu kila kitu (Wamitila 2003). Baadhi ya wahakiki wanasema kuwa, huyu msimulizi huwa na sifa za ki-ungu. Hii ni kwa sababu, huwa ana uwezo wa kupenya katika akili na mioyo ya wahusika wote.

Nadharia ya naratolojia pia huangazia kipengele cha wakati. Wakati ni kipengele muhimu katika simulizi yoyote. Ni katika wakati ambamo wahusika huishi, matukio hufanyika, na matendo ambayo ni kiini cha maudhui hutokea. Masuala yote katika

simulizi huhusiana na hadithi kwa namna moja au nyingine. Ni kwa sababu hii kipengele cha wakati kina nafasi muhimu katika simulizi inayokifanya kuhitaji kutafitiwa. Wakati hueleza ni lini ya hadithi. Vilevile hujibu suala la, 'kwa muda gani?' ama na 'mara ngapi?' Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* usimulizi maizi umebainika pakubwa katika Sura ya Kumi na Mbili katika maelezo ya Bwana Msa ambaye Bwana Msa ni mhusika maizi kwani anafahamu kadhia yote ile iliyotokea. Anafahamu kuwa, Ali Makame ndiye aliyeingia ndani ya nyumba ya Mwana wa Giningi na kuiba fedha na kisanduku cha dhahabu:

> Mengi nitakayokueleza hivi sasa ni mambo ya kukisia tu, maana sharti ukumbuke kuwa mimi sikuwapo mambo hayo yalipotendeka. Lakini unaweza kuyatia maelezo yangu akilini mwako uyapime binafsi kama yameelekea. (uk. 93)

Kupitia dondoo hili, ni wazi kuwa Bw Msa ni mhusika maize. Yeye anafahamu mambo mbalimbali na anayaweka wazi kwa hadhira ya msomaji kwa njia ya kushawizi. Hapa Bwana Msa ana uwezo wa kuona, kufuatilia na kuyaeleza mambo mbalimbali kwa wakati mmoja hata ingawa hakuwepo yalipotukia.

### 3.5 Hitimisho

Lengo la pili lililenga kudhihirisha aina ya usimulizi ambao mwandishi M. S. Abdulla anatumia katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.* Tulibainisha ya kuwa, M. S. Abdulla katika riwaya zake *Bwana Musa* ametumia pakubwa usimulizi wa nafsi ya tatu. Kupitia usimulizi huu, msomaji anapata kung'amua matukio yanavyofuatana vyema kiwakati. Isitoshe, usimulizi huu unamwezesha mwandishi kuwakuza wahusika wake kikamilifu na kubainisha ukuaji wao kimatendo na kiwakati. Pia, usimulizi huu unamwezesha msomaji wa kazi hizi kubainisha mbinu za lugha ambazo mwandishi huyu amezitumia ili kukuza dhamira na kuibua maudhui mbalimbali ya riwaya zake. Kupitia usimulizi huu, msomaji anapata kung'amua matukio yanavyofuatana vyema kiwakati bayana sana kwa kutumia jicho la msimulizi. Isitoshe, msomaji anabainishiwa na mwandishi namna wahusika wamesawiriwa na maadili wanayoyawakilisha kikamilifu pamoja na namna wanavyobadilika na hali zinazowaathiri kihulugha na kihali kiwakati. Utafiti ulibainisha ya kwamba, mwandishi aliitumia mbinu mseto za usimulizi katika ukuzaji wa dhamira na uibuaji wa maudhui katika riwaya zake.

# SURA YA NNE

# KUNGA ZA LUGHA KATIKA *KISIMA CHA GININGI* (1968) NA *KOSA LA BWANA MSA* (2007)

## 4.0 Utangulizi

Katika Sura ya Tatu, tulishughulikia dhana ya usimulizi na aina za usimulizi katika riwaya teule za M.S. Abdulla pamoja na athari zake katika mtindo, maudhui na fani. Katika Sura ya Nne, tumeshughulikia lengo la tatu la utafiti wetu. Lengo la tatu lilikuwa kudhihirisha namna kunga tofauti za lugha zilivyotumika katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa* kwa kutumia nadharia ya umtindo. Dhana ya umitindo hutumiwa kurejelea uhakiki wa lugha katika kazi za kifasihi pamoja na jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika matini za kifasihi (Wamitila 2003:39).

## 4.1 Matumizi ya Lugha Katika Kazi za Kifasihi

Lugha ni kiungo muhimu sana katika kazi za kifasihi. Mwandishi wa kazi ya kifasihi hutumia lugha kwa lengo la kukuza maudhui na dhamira katika kazi yake (Senkoro 1982:13). Mbinu hizi zinaweza kuwa tamathali za lugha pamoja na mbinu nyingine kama maswali ya balagha, miongoni mwa zingine. Tamathali za lugha hutumiwa ili kukoleza matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Kunga za lugha basi huhusishwa na namna mwandishi anakuwa mbunifu katika uandishi wake. Mbinu za lugha hufaulisha namna mwandishi anapitisha ujumbe kwa hadhira yake kwa njia ya kuvutia na kusisimua. Katika riwaya teule za M.S. Abdulla, mwandishi ametumia lugha kwa njia ya ubunifu ili kuwasilisha ujumbe wake. Ametumia kunga za lugha kama vile methali, takriri, tashbihi, tabaini, misemo, tashhisi, istiari na taswira kwa njia maalum ili kueleza mambo mbali mbali kiujumi na kwa njia inayowacha kumbukumbu kwenye fikra ya msomaji. Hizi ndizo baadhi ya tamathali ambazo tulishughulikia kwa kutumia nadharia ya umtido.

## 4.2 Matumizi ya Methali

Methali ni usemi mfupi wenye maana nzito au hekima ndani yake ambao hutumia lugha ya mkato ili kuonya au kusisitiza ujumbe (Hamadi 1981). Kwa mijibu wa King'ei na Ndalu, (2008) methali ni usemi mfupi wenye maana pana. Semi hizi huwa na busara pamoja na hekima. Huwa zinachipukia katika jamii fulani maalumu na huchukuliwa kuwa ni sehemu ya urithi wa jamii husika. Methali hutumiwa kwa nia ya kuelimisha, kuasa, kukejeli vitendo vibaya ama kudumisha mapisi na utamaduni.

Methali hutumiwa na watunzi wa kifasihi kupamba kazi na kufanya iwe ya kushawishi (Senkoro 1982: 21). Methali basi huweza kukoleza namna maudhui na dhamira huweza kumfikia msomaji kwa njia ya kisanaa. Methali pia hubainisha mazingira ya hadithi na kuonyesha maadili ya jamii ya mwandishi kisanaa. Aidha, methali hufanikisha mawasiliano na uhusiano wa wahusika katika jamii ya uandishi na namna wanatagusana katika maisha ya kila siku (Msokile 1992: 50). Methali ambazo hutumiwa katika kazi za kubuni kama vile riwaya, huwa na majukumu ya kuongeza msisitizo katika masuala yanayozungumziwa. Pia, huwafanya wasomaji wa kazi husika kuathirika kwa viwango mbalimbali kama inavyodhihirika katika riwaya teule za M S Abdulla.

### 4.2.1 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Thamani ya Kutenda Wema

Mwandishi M.S. Abdulla ametumia methali mbalimbali kutekeleza dhamira tofauti kama kuhimiza mahusiano mema baina ya wanajamii. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* Mwandishi ametumia methali kama: Anayekutaka mtake. (uk. 8)

Methali hii ilikuwa na kusudi la kuhimiza ushirikiano baina ya wahusika. Nadharia ya Umitindo inayoshughulikia namna lugha ya kitamathali iwezavyo kuibua maana mbalimbali katika kazi za kifasihi na namna matumizi hayo yanavyoathiri jinsi hadhira lengwa inavyoufasiri ujumbe huo. Methali hii ilitumiwa na Bw Msa baada ya kuipokea barua ya mwaliko kutoka kwa Spekta Seif akimwalika kuzuru Giningi. Mwandishi aliitumia kusisitiza dhamira ya mwito wa Spekta Seif. Inaibua taharuki na dharura ya wito huo. Kwa kufanya hivyo, inachangia kasi ya riwaya hii. Mawazo yao yanalingana kikamilifu na mawazo yetu kwamba methali ni kipengee cha lugha kilichosheheni mafunzo na elimu ya kijamii. Inachangia kuonyesha namna asasi ya polisi inaweza kushirikiana na wapelelezi wa kibinafsi kushinda uhalifu katika jamii.

### 4.2.2 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Imani za Kishirikina

Methali aidha zimetumiwa kuibua dhamira na maudhui ya imani ya wanajamii wa Giningi na kudhihirisha kuwa Wana-Giningi ni washirikina. Mwandishi anatumia methali: (uk. 52)

Methali hii ilitumiwa na mwandishi baada ya Bw Msa kumtembelea Fundi Mangungu ili kupeleleza madai ya kurogwa ya Mwana wa Giningi. Fundi Mangungu alimweleza kuwa ni mumewe Vuai ndiye aliyetaka kumroga. Kulingana na Leech

(1969:02), uchunguzi wa mtindo katika kazi za kifasihi huangazia jinsi ambavyo mtunzi wa fasihi hutumia lugha na mbinu nyingine katika kazi zake. Kupitia methali hii, dhamira ya imani za kishirikina inajitokeza wazi kwa msomaji na kuonyesha sababu ambazo zinamfanya Spekta Seif kuwa na shauku ya kumwita kwa dharura Bwana Msa.Hii ni kwa sababu wanajamii kwa kawaida huwa na hofu na waganga na hata huogopa kudai walichowapa. Methali hapa inampa mwandishi jukwaa la kujadili masuala ya kishirikina katika jamii hii bila kutumia maelezo mengi. Fundi Mangungu ni kielelezo cha imani hiyo potovu katika jamii hii. Kupitia kwa methali hii, maudhui kuhusu utamaduni na itikadi za kishirikina za jamii yanaendelezwa. Mwandishi anapinga imani na itikadi ambazo ni hasi na matokeo yake kijamii kama uchawi na kufanyiana mazingaombwe

### 4.2.3 Matumizi ya Methali katika Kufafanua Haja ya Kufanya Upelelezi Bora

Materu (1987) anaeleza methali kama msemo unaotumiwa kueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe adili, onyo au kusifu. Anaeleza: Mwiba uchomeako ndiko utokeako. (Kisima cha Giningi uk. 81)

Methali hii ina maana kuwa, utatuzi wa tatizo lolote hauna budi kuanza katika msingi wake na kujaribu kuufuatilia hadi mwisho wake. Kulingana na Nadharia ya Umitindo, kila rejista ina upekee wake wa kutumia lugha na ndio huibainisha kama sajili ama lugha ya mkutadha mahsusi. Methali hii imetumika kifasihi na mwandishi kuibua hali ya taharuki kwa msomaji. Msomaji hana budi kuwaza kuhusu chanzo cha matukio yanayojadiliwa. Methali hii ilitumiwa na mwandishi kuhimiza haja ya kufanya uchunguzi thabiti ili kuwanasa wahalifu katika jamii. Katika muktadha huu, Mwana wa Giningi ameuawa kisimani na ili kuanza uchunguzi wa mauaji hayo lazima waanzie pale kisimani. Pia, inasisitiza maudhui na dhamira ya upelelezi na kukomesha uhalifu kupitia asasi za vyombo vya dola. Vyombo vya dola vinakuwa kiunzi muhimu cha kuwasilisha ujumbe wake kwa umma.

### 4.2.4 Matumizi ya Methali Kutoa Nasaha kwa Wanajamii

Mwandishi aidha alitumia methali kusisitiza haja ya kuzuia mauaji ya wanajamii kwa kuchunguza kiini chake na kuwaadhibu wahusika. Katika *Kisima cha Giningi,* pia kuna methali: Mhini na mhiniwa njia yao ni moja. (uk. 90)

Methali hii ina maana kuwa mwenye kudhulumu na mdhulumiwa hatima yao ni moja. Msokile anashadidia mawazo ya Nadharia ya Umitindo anaposema ya kuwa, methali ni semi zinazotokana na ujuzi, sheria na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri na kufundisha mambo mbalimbali (Msokile 1992: 49). Kwa jumla ni semi fupi zinazotumia lugha ya mafumbo ili kuonya, kukosoa, kusisitiza na kuelekeza. Ukweli wake hutegemea jamii na mazingira maalum. Kulingana na Umitindo, msomaji wa matini ya kifasihi hana budi kuzingatia muktadha wa matumizi ili kubainisha mtindo uliotumika na kufafanua matumizi husika na maana zinazojibainisha na namna zinavyohusiana na ujumbe katika matini za kifasihi (Short, 2007). Bw Msa anamsimulia Spekta Seif kuhusu kisa kilichompelekea Ali Makame kufariki dunia. Inagunduliwa kuwa, Ali Makame ndiye aliyemuua Mwana wa Giningi ili arithi mali yake. Hata hivyo, anakufa maji na hatumii mali aliyoikamia. Mwandishi anaitumia methali hii kuendeleza dhamira na maudhui ya tamaa ya mali na haja ya kufanya kazi ili kujipatia riziki na mali badala ya kushiriki uhalifu na mauaji ya jamaa. Kando na kusisitiza dhamira ya kuonyesha jinsi jamii ilivyojaa watu wabinafsi, maudhui ya tamaa ya mali na mauaji pia yanaendelezwa na mwandishi, kwa matumizi ya methali mwafaka zinazoibua matukio ya hadithini na pia kuiasa jamii dhidi ya mielekeo potovu.

### 4.3. Misemo na Nahau

Misemo hutumia maneno ya kawaida kuleta maana isiyo ya kawaida (Senkoro 1982:25). Wamitila (2003) anasema kuwa, nahau ni misemo ambayo huwa na maana isiyo ya kawaida. Nahau basi huwa na maana nasibishi kimaana. Kwa mujibu wa utafiti huu, misemo na nahau huwa na dhima tofauti; husisitiza ujumbe fulani, hufunza maadili na kuongeza mvuto katika lugha. Kuna baadhi ya kunga hizi ambazo huhifadhi siri kwa kutumia tafsida. Kwa wasikilizaji na wasomaji, mbinu hii ya lugha huchochea hisia mbalimbali. Katika riwaya teule, mwandishi ametumia misemo kadhaa kwa ufasaha kulingana na utamaduni na mazingira yalikotokea.

#### 4.3.1 Matumizi ya Misemo Kueleza Ufanisi Katika Kilimo

Katika *Kisima cha Giningi,* mwandishi anaeleza kuwa, huenda kifo cha Mwana wa Giningi kilichochewa na ufanisi wake katika kilimo. Tunanukuu: …Mwana wa Giningi aliangusha nazi, miaka nenda miaka rudi. (uk. 15)

Msemo huu unaashiria ya kwamba, Mwana wa Giningi alikuwa na minazi mingi iliyozaa nazi nyingi na kumpa mazao mengi kwa miaka mingi. Umitindo hutumika kuelezea matumizi ya mitindo mbalimbali katika kazi ya kifasihi kwa njia ya kibunifu ili kuibua maana ya kina ya kitamathali (Simpson 2004:2). Kulingana naye, mtindo ni matumizi yanayombainisha mtunzi wa fasihi. Mwandishi wa kifasihi hutumia kazi ya kubuni kama jukwaa la kudhihirishia uwezo wake wa kutumia lugha katika mazingira mbalimbali. Mwandishi aliutumia msemo huu kusisitiza utajiri wa Mwana wa Giningi kama dhamira iliyomchochea ami yake kumuua.

### 4.3.2 Matumizi ya Misemo katika Kuzungumzia Masuala ya Urithi

Misemo pia ilitumiwa na mwandishi kukuza dhamira na maudhui kuhusu mauti yanayotokea katika jamii ya Giningi kutokana na urithi. Mwana wa Giningi, anawaza kuwa, mumewe Vuai aliingiwa na tamaa na:… kumfuata shetani. (uk. 23)

Kama alivyosema Leech kuhusu Umitindo, katika matini ya kifasihi, mtunzi huweza kukiuka hali ya kawaida na kutumia lugha kwa njia mpya na ya kipekee (Leech 1969:42). Msemo huu unaonyesha imani ya jamii kuhusu suala la urithi na jinsi suala hili linavyoibua mizozo na hata mauti katika jamii. Pia, msemo huu unaendeleza maudhui ya ushirikina. Tunaambiwa kuwa Fundi Mangungu alimwambia Mwana wa Giningi kwamba mumewe Vuai alijaribu kumroga ili afe ndipo arithi mali. Hii ndiyo sababu anamuwazia mumewe haya na hata kumshuku kuwa mwizi. Babake mzazi alikuwa amemtahadharisha kumwambaa ami yake na kukaa mbali naye.

### 4.3.3 Matumizi ya Misemo katika Kueleza Hali Anuwai za Kijamii

Tunaambiwa kuwa Idara ya Zaraa iliyohusika katika kujua majina na asili ya miti yote Giningi imejaribu kutafuta jina au asili ya mti ulioko kisimani bila mafanikio. Tunanukuu, Haikufua dafu. (uk. 65)

Imani hii inaashiria ya kwamba sayansi haihusiani na masuala ya kiitikadi na mara nyingine hushindwa kuyafafanua. Hii ndio maana mwandishi anatumia nahau kuibua mazingira ya kijamii na kuelezea imani zao kuhusu mazingira. Kimtindo, lengo la sanaa yoyote ile ni kumchorea mwanajamii taswira kamili ya mazingira yake kwa nia ya kumjuza na kumzindua kama asemavyo Harries (2009). Ili kufanikisha hali hiyo, msanii kupitia matukio na wahusika huweza kubuni lugha na mitindo mbalimbali ya kusawiria masuala yanayozungumziwa ili yamfikie msomaji wa matini husika kwa

njia inayobainika. Anachosema Harries ni kuwa, msanii mbali na kuwa na jukumu la kuifahamisha jamii kupitia maudhui. Namna maudhui hayo yanavyowasilishwa ni muhimu katika kuathiri hisia za hadhira lengwa. Ajabu kuhusu mti uliopo karibu na kisima cha Giningi inaashiria kina cha imani za kiitikadi katika jamii hii. Nahau basi ni njia ya mwandishi ya kufanikisha maelezo mwafaka ya kuiainisha jamii ya Giningi kwa msomaji wa riwaya hii.

#### 4.3.4 Matumizi ya Misemo katika Kueleza Hali ya Kuwekana Kimada

Katika Kosa la Bwana Msa, bibi aliyekuja kumwonya Jamila kuhusu mumewe anasema, Nimepata habari. Nimekuja hapa kukupa indhari uache *kuoga maji si yako*, wewe *unitokee kwa meno ya juu* na unijie kijuujuu kama moto wa kifuu. (uk. 9)

Katika dondoo hili, ‘kuoga maji si yako’ ina maana ya kujifaidi na kitu ambacho sio chako. Umitindo ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na wa kifasihi. Msemo huu umetumika na bibi huyu kumkanya Jamila kwamba Seyyid Ahmed bin Soud hakuwa mumewe bali alikuwa anamweka kinyumba tu. Msemo huu unamsaidia msomaji kugundua mgogoro baina ya wahusika.

### 4.4. Matumizi ya Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ambayo hutumiwa kuhusu vitu visivyokuwa na sifa walizo nazo watu hupewa sifa hizo (Senkoro 1982: 14). Vitu visivyo na uhai hupewa hulka za binadamu (Kuhenga 1977: 15, Msokile (1992: 55). Katika tamathali hii, vitu kama mimea, maji na viumbe vingi visivyo na uhai hupewa uwezo wa binadamu. Tashihisi hujengwa wakati ambapo tamathali zinazotumiwa hukusudiwa kuhawilishwa.

#### 4.4.1 Matumizi ya Tashihisi Kuonya Kuhusu Hulka na Ufuska

Mwandishi alitumia tashihisi kukashifu tabia mbaya katika jamii. Katika *Kosa la Bwana Msa*, tunanukuu:

> Na hayo ndiyo nisiyoyataka mimi yakufikie. Mtoto mwanamke hapo ulipo upite ukizurura majiani-mjini siyo shamba… na tena bado utakuwa usiku umekwishapiga hodi. (uk. 17)

Bwana Musa anamtahadharisha Jamila kuwa usiku ulikuwa umeshaingia. Mwandishi anatumia tashihisi *“usiku kupiga hodi”* ili kueleza usiku umefika na kwamba huenda kukawa na hatari (Leech 1969). Kulingana na Leech, kanuni za lugha ndizo zinazotumiwa kimtindo kuendeleza istilahi na kuzikuza miongoni mwa watumizi

mbalimbali wa kisanii. Usiku husababisha tabia hasi kama ufuska na mwandishi anatumia mbinu husika kubainisha maudhui ya ufuska na kuupinga.

#### 4.4.2 Matumizi ya Tashihisi Kueleza Hali ya Seyyid Ahmed

Tunaelezwa kuwa Seyyid Ahmed alipoamua kwenda Mazizini kumtafuta Jamila, alifunga safari kutoka Forodhani kwenda Mazizini kwa miguu. Alipofika huko alikuwa amechoka. Mwandishi anasema, Mgongo ulikuwa ukimtafuna na kiuno kikimpekecha. (uk. 123)

Mgongo umepewa uwezo wa kutafuna kama binadamu. Tashihisi hii inasisitiza uchovu aliokuwa nao Seyyid Ahmed. Mtindo ni upekee wa mwandishi na huwa na athari katika jinsi ujumbe unavyowasilishwa kwa hadhira husika (Leech 1969). Mwandishi basi alitumia msemo huu kuashiria umri mpevu wa Seyyid Ahmed na dhamira ya safari yao.

#### 4.4.3 Matumizi ya Tashihisi Kusisitiza Wingi wa Vyakula

Katika *Kosa la Bwana Msa* tunasoma:

> Tena chakula chenyewe! Hicho hapo mezani! Hutapindukia mipaka kama utakisia kuwa hata ile meza nayo, nafasi ya meza, iliyoandikwa juu yake chakula kile, ilikuwa ikimezea mate na ikitaasafu kimoyomoyo: *laiti kama ningalikuwa na mdomo kama wa binadamu*- kwa chakula hiki- kingenijia kijoyo kikanitia uchoyo na uroho, nikakila chote kabla wenyewe hawajaja kukila. (uk. 48)

Lengo la Umitindo ni kuchunguza tabia za lugha kwa madhumuni ya kudhihirisha sifa maalum zinazojibainisha kupitia miktadha ya kipekee kutokana na sifa za kijumla za kiisimu ambazo hudhihirisha miktadha ambamo matumizi husika ya lugha imetekelezwa (Crystal na Davy 1969: 10). Mbali na kuipamba lugha, mwandishi ametumia tashihisi hii ili kuonyesha vyakula vya kila aina na vingi ambavyo vilikuwa vimeipamba meza hiyo. Pia, anaitumia kuleta ladha ya utamu mdomoni kupitia maelezo yake.

#### 4.4.4 Matumizi ya Tashihisi Kutoa Maelezo kwa Kitafsili

Baadhi ya mbinu zilitumiwa na mwandishi huyu kuibua maudhui na dhamira zinazohusu uwajibikaji wa asasi za vyombo vya dola kama polisi. Katika *Kisima cha Giningi*, tunanukuu:

> Wenziwe na taa yao nyuma yake waliendelea na kuyafuata yale mashindo ya mbio, na walipofika pale pa kuingilia katika handaki upande ule unaoishia baharini, kurunzi yake Bwana Msa *iliwaokota watu wawili* wanapenya kwa urahisi katika lile handaki. (uk. 87)

Katika dondoo hili, tashihisi inajitokeza pale ambapo tunaambiwa kuwa kurunzi ya Bwana Msa *"iliwaokota watu wawili"* wakitoroka kwa kukimbilia handakini. Leech (1969) anatilia mkazo kwamba, lugha ya kiishara ama kitamathali aghalabu hutokana na watumizi wa lugha ya kawaida kutoka katika ukawaida huo na kuibua ukiushi na huo ndio huibua tamathali kama jazanda, taswira na tashbihi na nyinginezo. Asili ya lugha hiyo ya kitamathali na ambayo aliita Umitindo asili yake ni lugha ya mazungumzo tu. Anachosema ni kwamba, lugha ya fasihi chanzo chake ni lugha ya kawaida (isimu). Mwandishi anatumia mbinu hii kueleza haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu uhalifu na wahalifu.

### 4.5. Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo hufanya kitu kimoja, matendo ya kitu au vitu vyenye hulka mbalimbali, hulinganishwa na hali sawasawa ya maumbile (Kuhenga 1977: 6). Sitiari sawa na tashbihi hulinganisha vitu au watu lakini bila kutumia viunganishi linganishi (Senkoro 1982: 14). Sitiari kwa kawaida huhusisha matendo, vitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti (Msokile 1992: 53). Vitu na watu hulinganishwa na vitu na watu wengine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa. Katika riwaya teule, mwandishi ametumia sitiari kufafanua itikadi za kidini na za kishirikina na suala la urithi hasa katika *Kisima cha Giningi.*

#### 4.5.1 Matumizi ya Sitiari katika Kufafanua Imani za Kidini na Itikadi za Kishirikina

Mwandishi alitumia sitiari kulinganisha itikadi za kidini na za kishirikina katika jamii ya Giningi. Katika *Kisima cha Giningi*, tunaelezwa na Sheha kuwa uhusiano kati yake na ya Fundi Mangungu ulikuwa umeingia doa. Tunanukuu; Ulikuwa kama wa Paka na Chui (uk. 43).

Paka na chui ni wanyama wawili ambao wanaishi katika mazingira tofauti kabisa ya nyumbani na porini. Wanyama hawa hawapatani hata kuonana sawa na Fundi Mangungu na Sheha. Kulingana na umitindo, muktadha wa matini huibana lugha katika matumizi maalum na kuibua maana ya kipekee (Davy 1969:10). Lugha

hubadilika kutoka katika kiwango kilichozoeleka na kupata upekee unayoifanya kuwa mtindo mahsusi inapotumika katika mazingira tofauti na kwa lengo tofauti vilevile. Kwa mujibu wa nadharia hii, Fundi Mangungu anawakilisha imani potovu na hulka za udanganyifu ilhali Shehe anawakilisha maadili ya kidini. Mwandishi anatumia mbinu hii kubainisha hila za waganga katika jamii.

### 4.5.2 Matumizi ya Sitiari katika Kusisitiza Masuala Yanayoambatana na Urithi

Babake Mwana wa Giningi, Makame wa Makame anampa ushauri Mwana wa Giningi kabla ya kufariki kwake. Anamwambia,

> Kile kisanduku nilichokupa miaka ile unacho? Kiweke kitakufaa. Sikiliza wasia wangu. Baba yako mdogo, Ali Makame, ni ndugu yangu kwa baba na mama, lakini tahadhari naye. Nakuambia umwogope mtu yule na umwambae kama unavyomwamba jini au shetani; yule ni *sumu baridi*, usimwone vile, humjui wewe? (uk. 22)

Hapa, babake Mwana wa Giningi anamwonya mwanawe. Anamwonya dhidi ya babake mdogo na kumlinganisha na sumu baridi kwa sababu ya uovu wake. Istiari iliyotumika katika dondoo hili ni ‘sumu baridi.’ Sumu baridi ni mtu hatari na muovu. Inashadidia uovu wa Ali Makame na uhalifu. Hali hiyo inabainisha uoga wa Makame wa Makame kuhusu nduguye na madhara ambayo Ali Makame angemfanyia Mwana wa Giningi.  Mtindo hujibainisha pia katika dayalojia. Lugha ya kuzungumzwa kutegemea lengo, msemaji na mlengwa, inaweza kubeba maana ya ndani na hiyo ndiyo Leech anasema ni lugha ya kitamathali (Leech 1969). Mwandishi anaitumia mbinu hii kuashiria namna urithi katika jamii unavyoibua uovu hata kiasi cha kuua. Istiari hii inatilia mkazo kuwa babake mdogo Mwana wa Giningi hakuwa mtu wa kuaminika bali alikuwa hatari sana na mwenye tamaa ya mali. Kupitia mbinu hii, mwandishi anakuza hulka ya wahusika wa riwaya hii. Tunapata sifa za babake Mwana wa Giningi kwamba alikuwa mshauri mwema, mlezi mwema na aliyemjali mwanawe. Anamtakia Mwana wa Giningi maisha mema pindi atakapofariki. Ukatili wa Ali Makame pia unasawiriwa waziwazi kupitia istiari hii.

### 4.6. Matumizi ya Takriri

Mbinu ya takriri husisitiza kwa nia ya kutia nanga jambo fulani ili liweze kumwingia msikilizaji moyoni apate kulidhibiti vizuri (Kuhenga 1977: 35). Naye Msokile anaeleza takriri kuwa urudiaji wa maneno, silabi au sauti zinazolingana katika kazi za

sanaa (Msokile 1992). Mwandishi hutumia uradidi wa maneno au vipengele fulani kwa lengo la kusisitiza ama kulitia mkazo jambo linaloelezwa. Takriri hutumiwa kuipa hadithi mvuto wa kisanaa (Wamitila 2003).

### 4.6.1 Matumizi ya Takriri Kusisitiza Udhati wa Uchunguzi

Katika *Kisima cha Giningi*, Bwana Msa anapotafuta barua aliyoandikiwa na Spekta Seif ili amkabidhi Najum, mwandishi anatueleza kuwa, Bwana Musa aliinuka, kiko mdomoni, akaenda kupekua-pekua mezani. (uk. 7)

Crystal na Davy (1969:10) wanasema kuhusu umitindo kuwa, muktadha wa matini huibana lugha katika matumizi maalum na kuibua maana ya kipekee Lugha hubadilika kutoka katika kiwango kilichozoeleka na kupata upekee unayoifanya kuwa mtindo mahsusi inapotumika katika mazingira tofauti na kwa lengo tofauti vilevile. Wao waliangalia mtindo kiisimu na kusema kwamba, kanuni za kawaida za kiisimu ndizo hukiukwa ama kupindwa katika matini za kifasihi na kuibua lugha ya kitamathali ama kiishara (Short 2007). Kupitia mbinu hii tunagundua kuwa, wakati ambapo Bwana Musa alikuwa katika harakati zake za kumtafuta mwizi wa kisanduku cha dhahabu cha Mwana wa Giningi, mwandishi anatueleza kuwa Bwana Msa alikuwa akivuta toza yake huku akiangaza-angaza. (uk. 32) Takriri hii inaibua dhana kuwa, umakini unahitajika sana katika masuala ya upelelezi. Mwandishi basi anaitumia mbinu hii kuonyesha namna asasi za umma kama polisi wanavyolazimika kutafakari na kuwa makini ili kukusanya ushahidi na kuwanasa wahalifu.

### 4.6.2 Matumizi ya Takriri Kuibua Taswira Kamili ya Mandhari ya Kisimani

Katika ukurasa wa 70, mwandishi anatueleza picha ya mandhari kisimani na maiti ya Mwana wa Giningi ilipopatikana. Anaeleza:  Upande wa kushoto wa maiti, mtungi ulikuwa umetawanyika magae magae, na gae moja ya yale magae lilikuwa na majindari yake. (uk. 70)

Takriri inajenga taswira akilini mwa wasomaji kuhusu yale yanayoelezwa na mwandishi. Anaposema ‘magae magae’ msomaji anapata taswira ya mahali kulikojaa magae mengi. Msomaji wa matini ya kifasihi hana budi kuzingatia muktadha wa matumizi ili kubainisha mtindo uliotumika na kufafanua matumizi husika na maana zinazojibainisha na namna zinavyohusiana na ujumbe katika matini za kifasihi (Short 2007). Mbinu ya takriri imetumiwa kama njia ya kuipamba lugha na kusisitiza

dhamira ya kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uhalifu. Mbinu hiyo basi inamsaidia msomaji wa kazi husika kuelewa dhamira ya mtunzi kwa wepesi.

### 4.7. Matumizi ya Tabaini

Senkoro (1982: 16) anasema kuwa tabaini ni tamathali ya usemi ambayo kwayo maneno yanayokinzana hutumiwa katika sentensi ili kuleta msisitizo wa wazo ama mawazo yatolewayo. Msokile (1992) anaieleza tabaini kama usemi unaosisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani. Ni mtindo wa kupangilia maneno ili kuonyesha kuwa yanapingana kwa njia hiyo hiyo ya kusisitiza mawazo fulani. Wamitila (2003) anasema kuwa mbinu hii ni ya kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayoelekea kuonyesha msisitizo huo waziwazi. Aghalabu, matumizi ya mbinu hii ya usemi hutambulishwa na matumizi ya "si." M.S. Abdulla ametumia tabaini ili kuonyesha ukwasi wake wa lugha na kusisitiza ujumbe kulingana na dhamira yake. Mwandishi ametumia mbinu hii kueleza umbo la Spekta Seif.

#### 4.7.1 Matumizi ya Tabaini Kuelezea Umbo la Spekta Seif

Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* mwandishi anasema kuwa, Spekta Seif…alikuwa kijana mrefu, si mwembamba, si mnene; na kwa hivyo sare yake ya kazi ilimjaa vizuri mwilini na kumpa tambo la kupendeza. (uk. 13)

Tabaini hii inaeleza kuhusu umbo la Spekta Seif ambalo ni la wastani. Umitindo hutumika kuelezea matumizi ya mitindo mbalimbali kwa njia ya ubunifu ili kuibua maana fulani ya kitamathali (Simpson 2004:2). Mbinu hii imetumiwa na mwandishi katika riwaya teule ili kueleza umbo la askari na kimo kinachofaa katika kazi hiyo. Kupitia tabaini inakuwa wazi kuwa, msomaji anaweza kumtambua mhusika huyu na hata kumpenda kutokana na kile anachokiwakilisha katika jamii ya mwandishi.

### 4.8. Matumizi ya Tashbihi

Kuhenga anaieleza tashbihi kama mtindo wa uneni wa kifani, ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au kufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti na kuwa na mfanano au ushabihiano fulani wa hali ya utendaji au maumbile (Kuhenga 1977: 4). Kwa kawaida, tashbihi hutumia maneno kama; mithili ya, kama, sawasawa na maneno mengine ya kulinganisha ili kuonyesha dhana ya kufananisha vitu viwili au zaidi. Naye Senkoro anasema kuwa katika tamathali ya tashbihi, watu au vitu

viwili au zaidi hulinganishwa na watu au vitu vingine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa (Senkoro 1982: 14). Mbinu ya tashbihi hueleza sifa za kitu kinachozungumziwa, huongeza lugha ladha na kuonyesha umilisi wa lugha ya mwandishi. Mwandishi ametumia tashbihi kueleza maumbile ya Mwana wa Giningi na Ali Makame.

### 4.8.1 Matumizi ya Tashbihi Kueleza Maumbile ya Mwana wa Giningi

Katika *Kisima cha Giningi*, mwandishi anaeleza Mwana wa Giningi kama ifuatavyo: Mdomo wake mwembamba na kidevu chake chenye ncha kama yai kilionyesha utayari wa kusema yote yaliyo moyoni bila kubania. (uk.18)

Hapa kidevu kinapewa kinywa na kufanywa kuwa tayari kuzungumza. Kando na kulinganisha, tashbihi hii illitumiwa kutilia mkazo utayari wa Mwana wa Giningi kutoa ushahidi. Ulinganisho huo wa kidevu kuwa na umbo la yai pia ni ulinganifu unaompa msomaji picha kamili ya sura ya mhusika na kumbainishia hulka zake.

### 4.8.2 Matumizi ya Tashbihi Kueleza Maumbile ya Ali Makame

Mwandishi anatumia maumbile ya Ali Makame kumweleza ifuatavyo:

> Bwana huyo hutokwa na jasho jingi mno, mikononi na miguuni pia. Hutiririka ja vile maji ya mto. Chochote ashikacho huloa, hata hizo pesa aletapo huwa zimejaa jasho. (uk. 87)

Tashbihi hii ilitumiwa na mwandishi kuelezea umbo la Ali Makame ambalo kwayo halipendezi kwani mtu anayetokwa na jasho jingi huwa hafurahishi kukumbana na watu, ni mtu wa wasiwasi na huweza kuwa na harufu pia akiwa si mtu msafi. Picha inayosawiriwa hapa ya mhusika huyu inamchora kama mtu asiyependeza kumkaribia.

### 4.8.3 Matumizi ya Tashbihi Kuonyesha Umuhimu wa Uwajibikaji Kazini

Spekta Seif na Bwana Msa wanasikia mlio na mshindo wa miguu wa watu wakikimbia. Tunanukuu: Spekta Seif alifyatuka kama mshale. (uk.87)

Tashbihi iliyotumiwa inadhihirisha uwajibikaji wa Spekta Seif wa kukabiliana na uhalifu. Imetumiwa kuonyesha ujasiri wake kazini katika kudumisha usalama katika jamii ya Giningi. Mshale unaporushwa hufyatuka kwa kasi mno. Mwandishi anaitumii mbinu hiyo kubainisha kuwa Spekta alikuwa askari mzuri ila alipungukiwa na uwezo wa uchunguzi tu. Hali hiyo inatumiwa na mwandishi kimaksudi kubainisha

upungufu wa asasi ya polisi katika jamii huku ikiashiria ari ya askari wake walio na moyo wa kufanya kazi ipasavyo.

### 4.8.4 Matumizi ya Tashbihi katika Kutoa Nasaha

Mwandishi alitumia tashbihi kuonyesha namna jamii inavyotoa ushauri wa kinasaha kwa watoto. Anaeleza:

> Sikiliza wasia wangu. Baba yako mdogo, Ali Makame, ni ndugu yangu kwa baba na mama, lakini tahadhari naye. Nakuambia umwogope mtu yule na umwambae kama unavyomwamba jini au shetani; yule ni sumu baridi, usimwone vile, humjui wewe? (uk. 22)

Katika dondoo hili, Babake Mwana wa Giningi anamwonya dhidi ya babake mdogo. Analinganishwa na shetani au jini kwa sababu ya uovu na hivyo kutilia mkazo uovu wa Ali Makame.

### 4.8.5 Matumizi ya Tashbihi Kubuni Taswira ya Mizozo ya Kinyumbani

Mwandishi anatumia tashbihi katika *Kosa la Bwana Msa* wakati Bi. Shinuna alipokuja kumwona na kumwonya Jamila kuhusu mumewe. Tunaelezwa:

> Nimepata habari. Nimekuja hapa kukupa indhari uache kuoga maji si yako, wewe unitokee kwa meno ya juu na unijie kijuujuu kama moto wa kifuu. (uk. 9)

Dondoo hili linaonyesha hisia alizonazo bibi huyu na kuifanya hasira yake iogofye kama unavyoogofya moto. Moto wa kifuu ni hatari kwa sababu hukifanya kifuu kiwake kikiwa kimetumiwa kuhifadhi moto. Naye Bi Shinuna anafananisha hasira yake na moto iliomo kwenye kifuu kwa sababu huenda kikalipuka moto huo usipotolewa kifuuni kwa haraka.

## 4.9 Matumizi ya Tanakali za Sauti

Kuhenga (1977: 83) anaeleza kuwa katika taaluma ya lugha, tanakali za sauti pia hutumiwa kama mbinu ya lugha. Mwandishi hutumia tanakali za sauti kama lugha ya mwigo. Hutumiwa kubainisha asili ya vitendo vya viumbe ili kuingilia zaidi hamasa ya wasomaji na wasikilizaji.  Tanakali za sauti huunda taswira ya moja kwa moja kutokana na jinsi ambavyo mambo yanavyotukia (Senkoro 1982: 17). Tanakali mara nyingi hutokana na sauti ama maneno yanayofanana. Wakati mwingine, mfanano huu

hutokana na kurudiwarudiwa kwa neno au maneno Fulani na mwandishi katika kazi yake. Wamitila (2003) anasema mbinu hii hutumika kurejelea sauti ambazo huigiza jinsi kitu fulani kilivyo. Mwandishi ametumia tanakali za sauti kuelezea hulka za kipelelezi za Bwana Musa na haja ya asasi ya polisi kushirikiana na umma ili kufichua uhalifu.

### 4.9.1 Matumizi ya Tanakali za Sauti kueleza Hulka za Kiupelelezi za Bwana Msa

Katika *Kisima cha Giningi*, Bwana Msa anaposhuku kuwa kuna mtu nje walipokuwa ndani ya nyumba ya Mwana wa Giningi kuchunguza wizi wa kisanduku cha dhahabu anasikia miondoko ya mtu. Tunanukuu:

> Bwana Msa kwa ghafla alisimamisha kidole chake cha shahada katikati ya mdomo wake kuonyesha waliopo wanyamaze, na hapo alikwenda nyatunyatu mpaka mlangoni, akauvuta kwa ndani kwa nguvu. Wote waliokuwapo waliuona mlango ulivyokataa kunata, bali walisikia chuma kikigongana na tumbuo kwa nje – mlango umefungwa kwa nje na wao wako ndani. (uk. 32)

Kupitia dondoo hili, tunaona jinsi ambavyo Bwana Msa ni mwangalifu na msikilizaji mzuri wa kila kitu katika mazingira ya uhalifu. Tanakali hii inaonyesha taswira ya jinsi mambo yalivyokuwa. Kando na kuwachorea wasomaji picha na kuwafichulia jinsi tukio lilivyofanyika, tanakali ya sauti hii imefanya tukio hili lieleweke kwa urahisi. Mwandishi basi aliitumia mbinu hii kubainisha hulka ya kipekee ya Bwana Msa kama mpelelezi wa kibinafsi.

### 4.9.2 Matumizi ya Tanakali za Sauti Kuelezea Kilichojiri Pindi Mwana wa Giningi alipouwawa

Mwandishi anabainisha umuhimu wa ushahidi na mashahidi katika kutambua wahalifu katika kesi za jinai. Pandu anapoulizwa na Spekta Seif ikiwa alisikia chochote wakati Mwana wa Giningi alipouwawa kisimani. Tunaelezwa: La, sisi hatukusikia hata **kwi** baada ya kutoka Vuai. (uk. 76)

Katika dondoo hili, “kwi” inaonyesha hakukuwa na sauti yoyote ile hata kidogo. Tanakali hii ya sauti inasisitiza kwamba kulikuwa na ukimya wakati Mwana wa Giningi alipouliwa na yeye pamoja na wenzake Bwana Machano na Bwana Shame hawakusikia chochote. Mwandishi anaitumia kukuza dhamira ya mashahidi katika kesi ya jinai na namna wengi wanavyoshirikiana na wapelelezi kutatua kesi ya uhalifu

wa jinai. Pia inadhihirisha mipango ya Ali Makame alivyopanga kumwua Mwana wa Giningi ili atakapomvamia kusiwe na kelele yoyote jambo alilodhani litamfichia siri yake.

### 4.10 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi

Mbinu hii imetumiwa na mwandishi katika *Kisima cha Giningi* kurejelea suala la urithi. Wamitila (2003) anasema kuwa uzungumzaji nafsi ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea maongezi au hotuba ndefu inayotolewa na mhusika mmoja. Katika fasihi ya kibunilizi, Wamitila anasema uzungumzaji nafsi lazima uwe na dhamira ya kuukuza msuko yaani uwe na mchango katika tendo kuu la hadithi. Mbinu hii ya lugha huonyesha hisia tofauti za mzungumzaji na kuchora taswira kamili kuhusu kinachozungumziwa. Mwandishi anametumia mbinu hii kukuza maudhui katika *Kosa la Bwana Musa* kwa njia mbili kuu: Jinsi Jamila alivyotoroka na jinsi Seyyid Ahmed alivyopatwa na wasiwasi. Senkoro anashadidia Umitindo anaposema ya kwamba, kufaulu kwa mtunzi wa fasihi kupitisha ujumbe kikamilifu hutegemea uwezo wake wa kuisanii lugha na kuitumia kulingana na ujumbe unaolengwa (Senkoro 1988:6).

#### 4.10.1 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi Kueleza Kutoroka kwa Jamila

Katika *Kosa la Bwana Msa*, mbinu hii imetumika wakati ambapo Bwana Sheha anakuja nyumbani kwa Jamila ili aonane naye. Mwandishi anaeleza:

> Utatusamehe Bwana Sheha, bibie hayupo," alijibu Safinia kwa ukweli, huku akijiambia kimoyomoyo, kumbe wala hakwenda kwa Sheha kama tulivyotaka kufikiri. (uk. 24)

Hapa, Safinia ambaye ni Kijakazi wa Jamila anadhani Jamila yupo kwa Sheha. Kwa kutumia mbinu hii, mwandishi anafaulu kukuza matukio ya wahusika kama vile Jamila. Pia inatuacha katika taharuki kwani hatujui Jamila alipo. Hali hiyo inachangia kuongeza kasi ya riwaya na kuibua mvuto ndani ya msomaji wa kazi hizi teule na hasa katika kazi hii ambapo anapata ari ya kusoma zaidi ili ajue alikoenda Jamila.

#### 4.10.2 Matumizi ya Uzungumzaji Nafsi Kueleza Wasiwasi wa Seyyid Ahmed

Katika *Kosa la Bwana Musa*, Bwana Seyyid Ahmed yupo katika hoteli moja huko Chwaka. Amekodisha chumba hiki baada ya Jamila kugundua ujanja wake na hata kusababisha kutoroka kwake. Tunaelezwa:

> Lakini mimi sikufanya kitu ati! La, imesadifia tu, kuwa mahali pa ajali ya Shinuna ni pale pale nilipofikiwa mimi na hatari yangu- basi. Nini zaidi? Kwa hakika naogopa bure kutoka na kuonanana na watu. Hasa kwa hivi sasa, nina wajibu wangu wa kufanya kuhusu kifo cha marehemu Shinuna.… Basi, ni wajibu wangu kutoka niende nikashughulikie jambo hili. Lakini umesahau kama hupo Unguja, umesafiri, upo Nairobi? Lakini polisi na watu wengine wanajua kama sikusafiri, nipo hapa hapa nimejificha. Kama sikutoka mwenyewe kwa hiari yangu, nitakuja kuaziriwa humu humu pangoni mwangu. Ndiyo, lakini unajua kama kuna nini huko Chwaka kilichokuvuteni nyote wawili, wewe na Shinuna hata mkafikiwa na yaliyokufikeni? Tukifika hapo, basi na Jamila ataingia; na alivyokuwa hajulikani yuko wapi, itakuwa tuhuma na dhana mbovu upande wetu sote. Unasahau wewe- unasahau na yule Sheha wa huko Chwaka na maneno yake yale ya ukali aliyokutolea, maneno usiyoyajua mwanzo wala mwisho. Mradi mimi nakwambia Ahmed, umesimama juu ya kuti kavu! (uk. 92)

Dondoo lote ni uzungumuzi nafsia. Kupitia dondoo hili, Ahmed anawaza na kuwazua kuhusu matukio yanayomzingira hata akajipata katika hali yake. Anawaza kuhusu Jamila ambaye hajatua jicho kwake tangu atoroke kwake huku akiwaacha Siamini na Siajabu katika hali ya ukiwa. Anawaza pia kuhusu maafa yaliyompata; mkewe Shinuna kufariki na wajibu wake wa sasa kumpa heshima za mwisho. Kulingana na Leech, lugha ya kawaida inaweza kugeuka na kuwa lugha ya kifasihi sawa na anavyosema (Jakobson, 1960). Ni bayana kuwa Seyyid Ahmed ni mwongo. Alimdanganya mke wake Shinuna, kwamba alikuwa amepanga safari ya kuelekea Nairobi ilhali alikuwa Chwaka amekodisha hoteli. Uongo wake unamsababishia majuto. Katika uzungumzi nafsia huu tunachorewa hali kamili ya wasiwasi wa mhusika huyu pamoja na majuto aliyonayo.

### 4.10.3 Matumizi ya Uzungumuzi Nafsia Kumweleza Mwana wa Giningi Kuhusu Urithi

Katika *Kisima cha Giningi*, babake Mwana wa Giningi anamshauri Mwana wa Giningi na kumpa urithi. Anamrithisha shamba lake alilolizabuni kwa rupia elfu kumi na hata kumpa hati miliki ili kusiwe na mzozo baina ya Mwana wa Giningi na babake mdogo. Tunanukuu:

> Hapa ndipo Mwana wa Giningi alizikata fikra zake akawa anasema peke yake kidogo kidogo, Ah! Mimi sikumhini! Yeye mwenyewe tu, kawa na tamaa na kumfuata shetani, hata akaenda kuniroga kwa Fundi

> Mangungu ili nife apate kurithi! Ijapokuwa ndio wosia wa baba, lakini ndio nikae tu na adui kama huyo! (uk. 92)

Katika uzungumzaji nafsi huu, tunapata maudhui ya migogoro katika familia na uovu katika jamii. Hapa pia nafsi ya Mwana wa Giningi inazungumziwa na mgogoro wake na babake mdogo unawekwa wazi. Fikra za uchawi katika jamii hii pia zinazungumziwa kupitia uzungumzi huu na hivyo kumpa msomaji picha kamili ya fikra za jamii ya Giningi kuhusu ushirikina. Kauli hii pia inatutayarisha kwa kiasi fulani kuhusu uovu ambao Ali Makame anaweza kumfanyia mpwa wake. Kuhusu nadharia ya Umitindo, Leech anabainisha umuhimu wa muktadha katika kuteua matumizi ya lugha ambayo yanaafiki kazi fulani ya kifasihi kuhusiana na msuko wa vitushi na namna ya usimulizi katika kazi husika (Leech, 1969). Maudhui haya yanaendelezwa na babake mdogo Mwana wa Giningi; Ali Makame ambaye alimuuua mpwa wake kutokana na tamaa ya urithi na mali.

### 4.11 Matumizi ya Taswira

Wamitila (2003) anasema kuwa taswira hutumika kuelezea neno ama maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Anasema kuwa taswira zinaweza kuwa za kimaelezo; yaani maelezo yakaunda picha ambazo zinaashiria jambo fulani. Anasema kuwa kuna taswira ambazo huundwa kwa tamathali zingine za usemi hasa tashbihi au sitiari lakini anasisitiza kuwa taswira nyingi ni za uoni; zinazomchochea msomaji kuona picha fulani.  Mbinu ya taswira hujenga picha moja kwa moja katika akili za wasomaji na wasikilizaji. Kupitia mbinu hii, maudhui tofauti yatajitokeza. Mwandishi M.S. Abdulla ametumia mbinu ya taswira kwa ufanisi mkubwa mno. Mwandishi ametumia mbinu hii kuonyesha umuhimu wa uwajibikaji wa maafisa wa polisi na pia mandhari ya makazi tofauti ya Giningi.

#### 4.11.1 Matumizi ya Taswira Kuonyesha Uwajibikaji wa Maafisa wa Polisi

Katika *Kisima cha Giningi*, taswira imejengwa wakati ambapo Bwana Musa alipoenda kumwona rafikiye Spekta Seif. Tunanukuu:

> Spekta Seif alikuwa kashughulika kuitonogoa na kuitunga bustani yake iliyokuwa mbele ya nyumba yake kwa kuitilia maji na kuipalilia. Na keni lake la maji mkononi, alikuwa mara anatilia maji na mara anaihasi mimea yake ya tungule na nyanya iliyokuwa imekuja juu kwa nguvu baada ya mvua za

> rasharasha zilizonyesha mwezi uliopita. Kichwani mwake shungi la nywele za kipilipili lilikuwa bado halijachanwa na kuwekwa sawa kwa namna aitakayo mwenyewe. (uk. 10)

Katika dondoo hili, tunapata mandhari yaliyopo nyumbani kwa Spekta. Kabla Bwana Musa hajafika kwake anashughulika katika kusafisha bustani yake. Mwandishi anatumia taswira hii kubainisha udhaifu kwamba, wakuu wa vyombo vya dola wanatumia muda mrefu kwa shughuli za kibinafsi badala ya utumishi kwa umma.Taswira hii inayotuonyesha Spekta kuwa ni ni mtu nadhifu, mpenda mimea na mtunzi wa mazingira anamoishi.

### 4.11.2 Matumizi ya Mandhari Kuibua Tofauti za Kitabaka

Mwandishi anatumia taswira ya mandhari kuonyesha utabaka katika jamii ya Giningi. Wakati ambapo Spekta Seif na Bwana Msa wanakwenda kwa Mwana wa Giningi ili kujaribu kushughulikia kesi yake kwa kujionea makazi yake kidhahiri. Tunaelezwa:

> Baada ya kupita nyumba zinapata kumi walitokea kunako uwanja mkubwa na mbele yake nyumba yenye kuta ndefu na madirisha makubwa, paa lake la bati. Nje ilikuwa na baraza mbili, moja kubwa kwa upana na ya pili nyembamba ndefu iliyoko kwa nje. Mtu akifuata akili yake tu, itaweza kupotelea katikati kwa kufikiri kuwa nyumba hiyo, ikilinganishwa na nyumba zingine zilizo karibu, huweza kuwa ni kasri la mfalme imezungukwa na vibanda vya raia zake. (uk. 17)

Taswira hii inaelezea mahali anakoishi Mwana wa Giningi. Kutokana na maelezo haya kumhusu Mwana wa Giningi, ni dhahiri kuwa alikuwa wa tabaka la juu. Tunanukuu:

> Mwana wa Giningi alifungua mlango akasimama nje na mtungi wake mkononi. Herini zake za dhahabu masikioni, bangili zake nne za dhahabu mikononi, kipini chake cha fedha kikubwa kilichokuwa na nguvu za kuvuta nadhari za watu, na- kanga zake mbili mpya zinanukia udi- alisimama pale mlangoni, mwanamke mzuri na wa kupendeza. (uk. 18)

Mwana wa Giningi anasawiriwa kama mtu wa tabaka la juu kutokana na makazi na mapambo yake. Chumba cha Mwana wa Giningi pia kimeelezwa wakati ambapo Spekta Seif, Sajin Paolo na Bwana Musa walipoingia chumbani mwake tayari kuanza uchunguzi wao kuhusu wizi uliuofanyika mle. Tunanukuu:

> Hapo ukumbini na ujiani wa kuendea uani, sakafu yake ilikuwa ya saruji laini na kuta zake zilikuwa zikiwaka chokaa. Hapo

> ukumbini palikuwepo kitanda cha mayowe kilichotandikwa mkeka mzuri wa kili za rangi namna kwa namna. (uk. 18)

Kulingana na maelezo haya, Mwana wa Giningi alimiliki mali nyingi akilinganishwa na majirani zake. Tofauti ya kitabaka na ami yake inakuwa kichocheo cha uhasama kati yao. Kutokana na dondoo hili, jamii ya Giningi ilikuwa ya kitabaka na hilo lilichangia uhalifu.

## 4.12 Hitimisho

Kupitia lengo la tatu, tulibainisha ya kwamba, M. S. Abdulla katika riwaya zake za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa* anatumia kunga mbalimbali za lugha kuwasilisha ujumbe wake. Baadhi ya mbinu za lugha zilizotumikwa ni kama; taswira, methali, misemo, tashbihi, uhaishaji, istiari, takriri na uzungumzaji nafsi. Mbinu za lugha zimetumika kuipamba lugha, kusisitiza dhamira na maudhui kama upelelezi, mauaji, ushirikina na dhuluma dhidi ya mwanamke na urithi pamoja na upelelezi kupitia asasi ya polisi na wapelelezi huru. Pia, mbinu hizi zimetumika kama kipengele cha ploti. Sifa za wahusika zimebainishwa vyema kupitia kunga za lugha zilizotumiwa. Pia, zimewezesha wasomaji kuelewa kwa uwazi shabaha ya mwandishi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza msuko, usimulizi na matumizi ya lugha katika riwaya mbili teule za M. S. Abdulla: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007). Ni kutokana na umuhimu wa vipengele hivyo kifasihi katika kumtambulisha mwandishi na utunzi wake ndiposa tukateua kuchunguza baadhi ya kazi zake kama njia ya kudhihirisha namna vilivyochangia katika ufanikishaji wa uwasilishaji ujumbe katika riwaya teule.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo ya kudhihirisha aina ya msuko, kubainisha namna usimulizi ulivyoshughulikiwa, na kuonyesha matumizi maalum ya lugha katika *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Musa*. Katika Sura ya Kwanza, tulishughulikia msingi wa utafiti kwa kuchunguza usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia na mbinu za utafiti. Katika Sura ya Pili, tulishughulikia lengo la kwanza la utafiti wetu. Lengo la kwanza lilikuwa kudhihirisha aina za misuko ambayo mwandishi M. S. Abdulla anatumia katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Musa.*

Kupitia lengo la kwanza, tuligundua ya kuwa, M. S. Abdulla katika riwaya zake za: *Kisima cha Giningi* (1968) na *Kosa la Bwana Msa* (2007) anatumia misuko sahili, kioo na mwanzo-kipeo. Kupitia kwa misuko hii, mwandishi ameweza kudhihirisha maudhui mbalimbali waziwazi. Vilevile, mitindo hiyo imebainisha matumizi ya mbinu za lugha ya kisengerenyuma na taharuki kama mbinu muhimu katika uandishi wake. Isitoshe, misuko husika inachangia katika usawiri wa wahusika kimatendo na kiwakati katika riwaya husika. Dhima za wahusika na umuhimu wao unabainika vyema kupitia matumizi ya misuko hii. Pia imebainika ya kuwa, misuko hiyo inamwezesha mwandishi M. S. Abdulla kuwasilisha dhamira za riwaya hizi kikamilifu bila kumchosha msomaji kwa kutumia msuko wa aina moja. Kupitia kwa misuko hii, mwandishi ameweza kudhihirisha maudhui mbalimbali kibayana.

Kulingana na nadharia ya umtindo, malengo ya kazi ya fasihi husika ndiyo imemsukuma msanii kuteua mtindo fulani wa lugha. Aina ya usimulizi na msuko ndio huwasilisha ujumbe kwa njia ya kumwathiri msomaji wa kifasihi.

Kulingana na nadharia ya Umtindo, uchunguzi wowote unaohusisha msuko ni lazima uchunguze visababishi vya tukio la sasa. Mwandishi anatumia misuko kubainisha udhaifu wa vyombo vya dola kama asasi ya polisi ilivyopungukiwa katika kukabiliana na uhalifu katika jamii ya Giningi. Vuai anashikwa kwa kudhaniwa ndiye mhalifu. Hali hiyo hata hivyo inabatilishwa na tukio linalofuatia wakati Bwana Msa anasisitiza kuingia katika vyumba vya ndani katika kisima na kugundua maficho ya wahalifu.

Kupitia msuko sahili, tuligundua ya kwamba, mwandishi M S Abdalla anadhihirisha ya kwamba, matukio mbalimbali katika kazi za mtunzi huyu yanajengana na kukamilishana kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho. Katika riwaya teule, ilibainika ya kwamba, kimatukio, la pili litegemea tukio la kwanza nalo tukio la tatu linategemea tukio la pili kimfuatano. Msuko wa aina hii unajitokeza katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa.* Kulingana na nadharia ya Umitindo, kama wanavyoshadidia (Senkoro 1988, Leech na Short 1981), mbinu na ujumbe hufungamana. Tuligundua ya kwamba fani na maudhui ni vipengele ambavyo huenda sambamba na hutegemeana kwani wazo linalopitishwa linategemea jinsi linavyosimuliwa na mwandishi kama riwaya hizi zilivyoonyesha kupitia utafiti wetu.

Lengo la pili lililenga kudhihirisha aina ya usimulizi ambao mwandishi M. S. Abdulla anatumia katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.* Tulibainisha ya kuwa, M. S. Abdulla ametumia pakubwa usimulizi wa nafsi ya tatu. Kupitia usimulizi huu, msomaji anapata kung’amua matukio yanavyofuatana vyema kiwakati. Isitoshe, usimulizi huu unamwezesha mwandishi kuwakuza wahusika wake kikamilifu na kubainisha ukuaji wao kimatendo na kiwakati. Pia, usimulizi huu unamwezesha msomaji wa kazi hizi kubainisha mbinu za lugha ambazo mwandishi huyu amezitumia ili kukuza dhamira na kuibua maudhui mbalimbali ya riwaya zake. Isitoshe, msomaji anabainishiwa na mwandishi namna wahusika wamesawiriwa na maadili wanayoyawakilisha kikamilifu pamoja na namna wanavyobadilika na hali zinazowaathiri kilugha na kihali katika nyakati tofauti. Pia, usimulizi huu unamwezesha msomaji wa kazi za riwaye teule kubainisha mbinu za lugha ambazo

mwandishi huyu anazitumia. Utafiti ulibainisha ya kwamba, mwandishi aliitumia fani hii katika ukuzaji wa dhamira na uibuaji wa maudhui mbalimbali ya riwaya zake.

Lengo la tatu lilikuwa kudhihirisha kunga za lugha ambazo mwandishi M. S. Abdulla anatumia katika riwaya za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa.* Kupitia lengo la tatu, tulibainisha ya kwamba, M. S. Abdulla katika riwaya zake za *Kisima cha Giningi* na *Kosa la Bwana Msa* anatumia kunga mbalimbali za lugha kuwasilisha ujumbe wake. Baadhi ya mbinu za lugha zilizotumikwa ni kama; taswira, methali, misemo, tashbihi, uhaishaji, istiari, takriri na uzungumzaji nafsi. Mbinu za lugha zimetumika kuipamba lugha, kusisitiza dhamira na maudhui kama upelelezi, mauaji, ushirikina na dhuluma dhidi ya mwanamke na urithi pamoja na upelelezi kupitia asasi ya polisi na wapelelezi huru. Pia, mbinu hizi zimetumika kama kipengele cha ploti. Sifa za wahusika zimebainishwa vyema kupitia kunga za lugha zilizotumiwa. Pia, zimewezesha wasomaji kuelewa kwa uwazi shabaha ya mwandishi. Mwandishi anatumia lafudhi kudhihirisha sifa za wahusika kimazingira na nafasi zao katika jamii kwa kama anavyofanya mwana wa Giningi ama mhusika Fundi Mangungu. Kwa kufanya hiyo, dhamira ya mtunzi huyu katika kazi hizi inaeleweka kwa uwazi zaidi kwa msomaji. Kupitia lengo la tatu, ilibainika ya kuwa, kuna haja ya asasi za umma kuwajibika kikamilifu na kufanya upelelezi wa kina ili kuwashika wahalifu na kuipa jamii usalama. Pia, ilitumiwa na mtunzi kusisitiza maudhui na dhamira ya upelelezi na kukomesha uhalifu kupitia asasi za vyombo vya dola.

Uchunguzi wa msuko, usimulizi pamoja na mbinu za lugha kupitia utafiti wetu umedhihirisha ya kwamba, ili kuelewa riwaya za mwandishi huyu, kuelewa kipengelee cha fani na kunga za lugha ni njia mwafaka ya kubainisha dhamira na madhui katika uandishi wake. Kunga za lugha kwa wingi katika riwaya teule zimetumiwa ili kuibua msisimko na shauku ndani ya msomaji wa kazi za mwandishi huyu na basi kumpa utambulisho wa kipekee.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti uligundua ya kwamba, kazi za M S Abdalla zinatumia misuko changamano, usimulizi mseto pamoja na fani mbalimbali za lugha na wahusika ili kunasa makini ya msomaji na kudumisha dhamira ya uhalifu na upelelezi. Aidha, mbinu hizi mseto zilitumiwa kimaksudi kwa lengo la kuongeza kasi katika matukio na kukuza taharuki na hamu ndani ya msomaji.

## 5. 4 Mchango wa Utafiti

Kwa kuchunguza fani, utafiti huu umewezesha uelewekaji wa kina wa riwaya teule za mwandishi huyu na vilevile kuwekea msingi wasomaji na wahakiki wa kazi za kipelelezi wa baadaye kuhusu mchango wa fani katika kufanikisha kazi za kipelelezi.

## 5.5 Mapendekezo

Suala letu lilikuwa la kifasihi na lilijikita katika uchunguzi wa vipengele vichache vya fani na lugha. Kwa watafiti wa baadaye tunapendekeza wamchunguze mwandishi huyu kwa mtazamo wa kiulinganishi kwa kumuliko vipengele tofauti za fani kama vile wahusika. Watafiti pia wanaweza kuchunguza sifa yoyote ya kazi zake kwa kutumia nadharia tofauti na zile ambazo tumezitumia.

## MAREJELEO


Baldick, C. (1990) *The Concise Oxford dictionary of literary terms.* Oxford University Press.

Bradford, R. (1997) *Stylistics.* London: Routledge.

Carpenter and Neumeyer, (1975) *Teaching the short story*. Plot University of Illinois press.

Crystal, D. & Davy, D. (1996) *Investigating English Style.* London: Longmans, Green and Co. Limited.

Genette, G. (1980) *Narrative Discourse: An Easy in Method.* Ithaca: Cornell University Press.

__________ (1982) *Figures of Literature Discourse. Alan Sheridan (tran).* Blackwell: Oxford.

Hawthorn, J. (1987) *Unlocking the Text: Fundamental issues in Literary Theory.* London: Edward Arnold.

Harries, K. (2009). *Hegel's Introduction to Aesthetics.* Yale University, Fall Semester.

Jakobson, R (1960) *Linguistics and Poetics*: Thomas A. Sebeok (mhr) *Style in Language.* Cambridge: MIT Press, iliyochapishwa katika J-J Weber (mhr) *The Stylistic Reader*: London.

Kairu, M. W. (2005) *'Uhalisia na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto.'* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kitsao, J. (1975) *A Stylistic Approach Adopted for the study of Written Swahili Prose Texts.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kombo, D. K. & Tromp, D. L. A. (2006) *Proposal and Thesis writing*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kujenga, C. (1977) Tamathali za Usemi: Mtalaa wa Kiswahili. Nairobi: East African Literature Bureau.

Leech, G. N. (1969) A *Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman Group Limited.

Syambo, B. K. na Mazrui, A. M. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East African Publishers.

Matundura, E. (2007) *Taswira dumifu za uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.* Nairobi: University of Nairobi. Tasnifu ya uzamili. Haijachapishwa.

Matteru M. L. B. (1987) *"Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi" Mulika namba 19*. Dar es Salaam.

Mlacha, S. A. K & Madumulla, J. S. (1991) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar-es-salaam: Dar es Salaam University Press.

Mbuthia E. M. na P. I. Iribemwangi (2014) *Analysis of Stylistic Trends in Published Kiswahili Short Story Genre.* Journal of Education and Practice www.iiste.org ISSN 2222-1735 (Paper) ISSN 2222-288X (Online) Vol.5, No.8, 2014 32.

Mogambi, K. (1983) *Uhakiki wa Hali ya Wanyonge Katika Riwaya Tatu za S. Mohammed.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Musembi, N. (2008) *Matumizi ya Taswira na Ukinzano kama Kichocheo cha Zinduko katika riwaya za G. K. Mkangi. Mafuta (1984) na Walenisi (1985).* Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa).

Mohamed S.A (1990) *Ulimwengu wa Mwandishi wa Kiswahili Kilugha.* katika Mbatiah (Mhr*) Mwamko*

Mohamed S. A. (2010) *Damu Nyeusi na Hadithi Nyi*ngine: Nairobi. Moran publishers.

______________ (1990) *Kivuli Kinaishi*: Nairobi. Longhorn publishers.

_____________ (1995) *Amezidi*: Nairobi. East African Education Publishers.

____________ (1995) Mtindo *katika Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*: Nairobi. East African Educational Publishers.

Mohochi, E. S. (2000) *Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini*. Nordic Journal of African Studies 9(2): 49-59. University of Egerton, Kenya.

Msokile, M. (1993) *Miongozo ya Lugha ana Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*, Dar es Salaam: DUP.

Muhando, P. na Balisidya, N. (1976) *Fasihi na Sanaa za maonyesho*. T.P.H. Dar es Salaam.

Ndalu, A. na King'ei K. G. (1989) *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndung'u, N. (1996) '*Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi'.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oiro, G. O. (2017) *Urudiaji na Uwasilishaji wa Maana katika Ushairi wa Kisiasa.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ongarora, S. (2007) '*Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine'.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oyoyo, O. J. (2013) *'Uhakiki wa fani katika ngano tano za Kiswahili.'* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Raglan, Fitzroy R. Somerset, Lord (1936). *The Hero: A Study in Tradition, Myth, and Drama*. Westport, Ct.: Greenwood Press 1975.

Rimmon-Kenan, S. (1983) *Narrative Fiction: Contemporary Poetics.* London: Routledge.

Short, T. L. (2007) *Pierce's Theory of Signs*. Cambridge: Cambridge University Press.

Senkoro, F. M. K. (1982) *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Simpson, P. (2004) Stylistics*: A resource Book for Students.* London: Routledge.

Njogu, K na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyetta Foundation.

Wallek, R. na Warren, A. (1965) *Theory of Literature.* London: Jonathan Cape.

Wamitila, K. W. (2003) *Uhakiki wa Fasihi, Msingi na Vipengle Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.